




**VIGOGO** wa TASAC watimuliwa kikao Kamati ya Bunge

UK. 4


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Wilaya inavyoibuka kimikakati kwenye sayansi, yaandaa wasomi sekondari
Mabinti wanapompata miezi mbadala kuzikabili mimba, utoro
Kasi kubwa ya UVIKO-19 ni maswali zaidi ya majibu
SAYANSI
NA ADELA MADYANE, KIGOMA
**Baadhi ya 'zawadi' anazopata mtoto unapomsafirisha ili akatumikishwe**
• Ulemavu, sonona, majeraha na makovu

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Agosti 24, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580682

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# Sirro kunguruma kesi ya Mbowe

**Sabaya** naye atajwa, Jamhuri kupeleka mashahidi 23, vielelezo 19... *Uk. 2*




Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kuwasili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi ya ugaidi inayomkabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Askofu Gwajima awekwa kikaangoni kwa saa mbili

UK. 2



Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima (kushoto), akibadilisha kiti alipofika mbele ya wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, waliomuita kwa ajili ya kujibu tuhuma mbalimbali zinazomkabili ikiwamo kusema uongo na kushusha hadhi na heshima ya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



AZARIA SIVONIKE · BENARD MUSHINGI · JOEL MITONDWA · FAHADI HAJI · SAIDI BUDDY

# Chanzo cha ajali iliyoua maofisa watano wa TRA chawekwa bayana

UKURASA 3

**MICHEZO** SERIKALI YAWEKA KIPORO USAJILI LIGI KUU UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Sirro, Sabaya watajwa kesi ya Mbowe

**NA KULWA MZEE**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, wametajwa kuwa mashahidi wa upande wa utetezi katika kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe.

Wakati hao wakitajwa upande wa utetezi, Upande wa Jamhuri umedai kuwa mashahidi 23, akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz, watatoa ushahidi kuijenga kesi hiyo.

Katika maelezo ya mashahidi yaliyosomwa jana, Jamhuri ilidai kwamba Mbowe ni kinara katika njama za kufanya vitendo vya kigaidi, kuwadhuru viongozi wa serikali ikiwamo kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Sabaya. Maelezo hayo yalisomwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Jamhuri inawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, Jenitreza Kitali na Esther Martin wakati Mbowe na wenzake watatu wanawakilishwa na mawakili Peter Kibatala, John Mallya, Jebra Kambole, Frederick Kihwelo, Lwekamwa Rweikiza na Marie Mushi.

Wakili Katuga alidai Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) aliwasilisha taarifa Agosti 17, mwaka huu, ili washtakiwa wasomewe maelezo ya mashahidi na kesi ihamie Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Hakimu Simba aliruhusu mashtaka kusomwa na Wakili Katuga aliwataja washtakiwa kuwa ni Mbowe, Halfan Bwire, Adam Kasekwa, maarufu kama Adamo na Mohamed Lingwenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa wanadaiwa kula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi, mwaka jaja, katika Hoteli ya Aishi, Manispaa ya Moshi, Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta, kuhatarisha usalama wa taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Shtaka la pili, wote wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi ambavyo vilimsababishia majeraha Sabaya na shtaka la tatu Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na maeneo hayo, aliwawezesha kifedha Halfani, Adam na Lingwenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia kufanya ugaidi kwa kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Tanzania.

Shtaka la nne, washtakiwa wote wanadaiwa kushiriki vikao vya kufanya vitendo vya kigaidi wakati shtaka la tano, Adama anadaiwa Agosti 5, 2020 eneo la Rau, alikutwa na bastora yenye namba A 5340 aina ya Luger.

Mshtakiwa Halfani anadaiwa Agosti 10, 2020, kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi, alitumia sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa(JKT) ambazo ni suruali moja ya JKT na suruali nne za JWTZ, fulana moja, koti la mvua, jaketi, kofia tano, ma- 'overall' matano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha maji na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote mali ya JWTZ.

Katika kesi hiyo, Jamhuri ilidai kuwa mbali na mashahidi 23, itawasilisha vielelezo 19 vya maandishi.

Katika ushahidi wa Kamishna Boaz uliosomwa na Katuga, ulidai kuwa Julai, 2020 alipokea simu kutoka kwa mtu aliyejitambulisha kuwa ni Luteni Dennis Urio, alimwambia kuna uhalifu umepangwa kufanyika kwa ajili ya kudhuru viongozi wa serikali.

Alidai kuwa mtu huyo alimwambia aende ofisini kwake na walikwenda kisha akampa taarifa kuwa Mbowe anataka amtafutie wanajeshi wastaafu, makomandoo au waliofukuzwa kazi ili ashirikiane nao kuwadhuru viongozi akiwamo Sabaya.

Baada ya kuambiwa hivyo, Boaz anadaiwa kumwambia Luteni Urio asijitoe bali aendelee kumtafutia watu na alimtafutia watu wawili. Alidai kuwa mpango wa kumdhuru Sabaya ulikamilika, watuhumiwa walikamatwa mkoani Kilimanjaro na baada ya kufanya upelelezi, walibaini kuwa Mbowe ndiye kinara wa mpango huo.

Pia ilidaiwa kuwa Kamishna Msaidizi (ACP) Ramadhani Kingai aliitwa na Boaz kwa ajili ya kusikiliza maelezo ya Urio aliyotoa kuhusu mpango wa Mbowe na kwamba Urio aliwatafuta watu wawili akawaunganisha na Mbowe na kijana mmoja akamfanya kuwa mlinzi wake.



Msongamano wa vibanda vya wafanyabiashara wadogo maarufu machinga hadi kuziba eneo la waenda kwa miguu katika eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa wapita njia na vyombo vya moto. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Gwajima awekwa kikaangoni saa mbili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kawe (CCM), Askofu Josephat Gwajima, amewekwa kikaangoni kwa saa mbili na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, huku akikataa kukalia kiti na kutumia kipaza sauti kilichokuwa kimewekwa kwa ajili yake.

Askofu Gwajima alihojiwa na kamati hiyo kufuatia maelekezo ya Spika wa Bunge, Job Ndugai aliyoyatoa Agosti 21, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa ya wito huo, Askofu Gwajima alitakiwa kufika mbele ya kamati kwa mujibu wa kanuni ya 4(1)(a) na (b) ya nyongeza ya nane ya kanuni za kudumu za Bunge toleo la Juni 2020 ambayo inaipa mamlaka kamati hiyo kuchunguza mambo yanayohusu maadili ya wabunge yanayopelekwa kwa Spika.

Mbunge huyo aliingia kuhojiwa saa 8:43 mchana na kamati hiyo chini ya Mwenyekiti wake Emmanuel Mwakasaka yenye wajumbe zaidi ya 20 na kumaliza mahojiano saa 10.50 jioni.

Kabla ya kuingia ukumbini, Askofu Gwajima alionekana akisali muda mwingi katika eneo la utawala alilokuwa amekaa akisubiri kuitwa kuingia ndani ya ukumbi.

Hata hivyo, alipotakiwa kuingia ndani ya ukumbi aliomba asubiriwe anywe dawa ambazo alimwagiza dereva wake kuzifuata kwenye gari, wakati akiwa nje, Mwenyekiti Mwakasaka aliwaeleza wajumbe kuhusu taarifa hiyo huku akidai wanamsubiri anywe dawa licha ya kuwa hakuwa na taarifa za ugonjwa wake.

Alipoingia ndani aligoma kukalia kiti na kipaza sauti kilichokuwa kimewekwa kwa ajili yake ndani ya ukumbi wa mahojiano.

Mwenyekiti Mwakasaka alikubali ombi lake na kueleza ni kitu ambacho hakina shida kwa kuwa ana haki ya kufanya hivyo.

Mwakasaka alisema tayari Askofu Gwajima ametii wito na kuwataka waandishi wa habari kutoka ndani ya ukumbi kwa kuwa wanaanza mahojiano rasmi.

"Baadaye baada ya kikao kumalizika waandishi mtaulizа kila kinachofuata, waandishi tunaomba mtupishe," alisema Mwenyekiti huyo.

Katika viwanja vya bunge, Mbunge huyo aliwasili saa 12:36 mchana na gari lenye rangi nyeusi namba T 173 DHA na kupokelewa na askari wawili mmoja akiwa amevaa sare na mwingine akiwa amevaa kiraia.

Getini alilazimika kukaguliwa mara tatu kutokana na mashine ya ukaguzi kulia kila alipokuwa akipita.

Akiwa getini aligoma kuvaa barakoa na alipoulizwa sababu na kutovaa alijibu kuwa ana mzio wa kushindwa kupumua.

## HABARI KITAIFA

# Chanzo ajali iliyoua maofisa TRA bayana

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI



Mabaki ya gari lenye namba za usajili STL 8825, walilokuwa wakitumia maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), baada ya kupata ajali katika eneo la Hanseketwa, wilayani Mbozi, mkoani Songwe jana na kusababisha vifo vya maofisa watano wa mamlaka hiyo. **PICHA: NEBART MSOWA**

WATUMISHI watano wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) wamekufa papo hapo baada ya gari aina ya Toyota Landcruiser lenye namba za usajili STL 8825 walilokuwa wakilitumia kufanya doria, kugonga lori lenye namba za usajili T. 586 ANE aina ya Mitsubishi Fuso kwa nyuma katika eneo la Hanseketwa wilayani Mbozi.

Ajali hiyo ilitokea jana majira ya saa 11:00 alfajiri, wakati maofisa hao wakiwa wanafukuzia gari lingine lililodhaniwa kuwa lilikuwa likisafirisha bidhaa za magendo kutoka Tunduma kwenda Mbeya ambalo bado halijafahamika.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi (ACP), Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kwamba miili ya watumishi hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Songwe, iliyoko Vwawa, wakati taratibu zingine zikiendelea.

Alisema katika maofisa hao kati yao wanne ni wafanyakazi wa TRA Mkoa wa Mbeya na mmoja ni mtumishi wa mamlaka hiyo Mkoa wa Songwe.

Kamanda Magomi aliwataja waliopoteza maisha kwenye ajali hiyo kuwa ni dereva Azaria Shifonike, Joel Mitondwa, Saidi Buddy, Fahad Hassan wote watumishi wa TRA Mbeya na Benard Mashingi ambaye ni wa Songwe kituo cha Tunduma.

"Chanzo cha ajali hii ni mwendokasi wa gari la TRA ambalo lilikuwa likifukuza gari lingine, lakini likaingia nyuma ya lori na kusababisha maofisa hao kupoteza maisha na walikuwa wakitimiza majukumu yao," alisema.

Magomi alitoa wito kwa madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani, ili kuepusha ajali zinazoweza kuzuilika na kuokoa maisha ya abiria pamoja na watumiaji wengine wa barabara.

"Sheria ni msumeno. Natoa wito kwa madereva wetu bila kujali kama ni wa magari binafsi au yale ya serikali, wote wanatakiwa kuzingatia na kufuata sheria za usalama barabarani kuepusha ajali kama hizi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary mgumba, na baadhi ya maofisa wa TRA waliofika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Songwe, waliangua kilio baada ya kujionea miili ya maofisa hao ikiwa imehifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhia maiti.

Mgumba alitoa pole kwa ndugu, jamaa wa marehemu huku akiwataka wawe watulivu wakati serikali ikiendelea na taratibu zingine zikiwamo za kuandaa maziko ya maofisa hao.

Aliwataka madereva wa magari ya serikali kuzingatia sheria kama ilivyo kwa madereva wa magari ya watu binafsi kwa kuwa wote wanaongozwa na sheria za aina moja.

# Mawakili wa Sabaya wakwaa kisiki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imetupilia mbali pingamizi la mawakili wa utetezi katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai ole Sabaya na wenzake wawili kutaka maelezo ya mshtakiwa wa pili, Sylvester Nyegu (26) yasitumike katika kumhoji.

Kutokana na kutupiliwa mbali huko, mahakama imekubali maelezo hayo aliyoyaandika polisi yatumike katika kumhoji hata kama haijathibitishwa kuwa ya ukweli.

Akitoa uamuzi mdogo jana mahakamani hapo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amwora alisema hoja za maswali ya dodoso (mahojiano) hazina kikomo, hivyo mshtakiwa huyo ambaye ni shahidi wa utetezi, anaweza kuulizwa maswali yoyote kwa kutumia kifungu cha 154 cha Sheria ya Ushahidi.

"Hivyo naruhusu wakili wa serikali kuendelea na maswali ya dodoso na shahidi huyu," alisema hakimu.

Kabla ya kutolewa uamuzi huo, Agosti 20, mwaka huu, Hakimu Odira aliahirisha kusikiliza kesi hiyo baada ya mawakili wa utetezi kupinga uhalali wa wakili wa Jamhuri kumhoji shahidi huyo kupitia maelezo yanayodaiwa aliandika kituo cha polisi, hivyo kuzua mvutano wa kisheria.

Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, alimhoji shahidi huyo kama hakuwahi kuandika maelezo yoyote kituo cha polisi wala kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na kukataa kuhojiwa wala kuandika maelezo yoyote.

Kutokana na maelezo hayo, Wakili Kweka aliiomba mahakama kutumia kifungu cha 154 cha Sheria ya Ushahidi, kutumia maelezo ya ushahidi aliyoandika kituo cha polisi. Baada ya kutolewa kwa uamuzi huo, Wakili Kweka aliendelea kumhoji shahidi huyo na sehemu ya mahojiano hayo ilikuwa kama ifuatavyo:

**Wakili:** Kabla ya kufanya jambo lolote unamtanguliza Mungu ni sahihi na imani yangu kabla hujaja hapa ulisali.

**Shahidi:** Ndiyo

**Wakili:** Nilikuuliza maswali katika nyaraka kwenye maelezo yako ya polisi yanafanana na ya hapa?

**Shahidi:** Havifanani

**Wakili:** Wakati unafikishwa TAKUKURU ulikuwa na miaka mingapi?

**Shahidi:** Miaka 27

**Wakili:** Katika Halmashauri ya Hai ulikuwa nani?

**Shahidi:** Nilikuwa najitolea kuanzia Februari, 2020 hadi Mei 27, mwaka huu, nilipoitwa TAKUKURU.

**Wakili:** Kuna kesi nyingine ya uhujumu uchumi namba 27 ya mwaka 2021 mnashtakiwa wote, wewe na shahidi namba moja (Sabaya).

**Shahidi:** Siwezi kulizungumzia hilo.

**Wakili:** Wewe ulikuwa unajitolea wapi?

**Shahidi:** Ofisi ya Idara ya Kilimo pale kwa mkurugenzi.

**Wakili:** Kwa nini wewe tu ndiye unahusishwa na Mkuu wa Wilaya (Sabaya) tena katika kesi mbili tofauti wakati mpo wengi watumishi wa kuajiriwa na kujitolea?

**Shahidi:** Hilo sifahamu?

**Wakili:** Kuletwa kwako mahakamani ni baada ya mkuu wa wilaya kutenguliwa?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** PW 6 (shahidi wa sita wa Jamhuri) aliyekuja kutoa ushahidi upande wa Jamhuri mnafahamiana naye au una ugomvi naye?

**Shahidi:** Sifahamiani naye wala sina ugomvi naye.

Baada ya mahojiano hayo na kuongozwa na mawakili wake wa utetezi, alimaliza ushahidi wake na shahidi wa tatu Daniel Mbura alianza kutoa utetezi wake.




**TANZIA**

**ELIZABETH JUBILATE MUNISI**

**(KUZALIWA 25-12-1940 KUFARIKI 18-08-2021)**

Familia ya Marehemu Jubilate Munisi inasikitika kutangaza kifo cha mama yao, Elizabeth Jubilate Munisi kilichotokea tarehe 18 August 2021 katika hospitali ya Arusha Lutheran Medical Center.

Mazishi yatafanyika siku ya Alhamisi, tarehe 26 Agosti 2021, huko Machame na familia inaomba na kusisitiza taratibu za kuepuka misongamano pamoja na kuvaa barakoa zifuatwe kwa dhati.

Ratiba yote ya mazishi itatolewa kwa wahusika wote.

**JINA LA BWANA LIHIMIDIWE**

216419702

# DC ataka motisha viwanja, si barua

**Na Lilian Lugakingira,**

**MULEBA**

MKUU wa Wilaya ya Muleba, Thoba Nguvila, ameagiza walimu ambao masomo yao yataongoza kiwilaya katika mitihani ya taifa ya darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita kupewa viwanja kama motisha, badala ya barua za pongezi.

Amesema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha ufaulu unaongezeka wilayani hapo.

Nguvila alitoa agizo hilo, wakati akikabidhiwa matangi manane ya kuvunia maji ya mvua, matundu 24 ya vyoo na vyumba vinne vya madarasa, vilivyojengwa na Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera kupitia miradi wa Ruhita AP na Mbuka AP, kwa gharama ya Sh. milioni 305.1.

Alisema ili kutimiza azma hiyo, mwaka huu wanatenga viwanja tisa kwa ajili ya walimu, ambao masomo yao yatashika nafasi ya kwanza hadi ya tatu na kwamba hatua hii itawafanya walimu kuwa na ushindani katika ufundishaji.

"Walimu hatuwezi kuendelea kuwa na zawadi ya kuwaandikia barua tu za pongezi kwamba hongera mwalimu. Ina maana akiongoza mara 30 ajaziwe barua 30 ofisini, kwani atakula barua? Lakini mwalimu akiwa na kiwanja na kujenga nyumba ni kumbukumbu nzuri kwake na kwa familia yake kuwa alifanya kazi nzuri," alisema.

Akikabidhi miundombinu hiyo na matangi ya maji vilivyonufaisha shule za msingi tisa ambazo ni Nyakatanga, Kishuro, Burungura, Mtulange, Nyarugando, Kakoma na Nyakishozi zilizoko chini ya mradi wa Ruhita AP na Kangoma na Bushekya zilizoko chini ya mradi wa Mbuka AP, Mkurugenzi wa Rasirimali Watu wa shirika hilo, Joan Kiiza, alisema lengo ni kupunguza msongamano darasani na kulinda afya za wanafunzi.

"Kati ya Sh. milioni 183.1 zilizotumika kununua matangi ya maji, kutengeneza miundombinu ya maji na kujenga matundu 24 ya vyoo katika shule saba za msingi chini ya mradi wa Ruhita AP, wananchi walichangia Sh. 840,000," alisema.

# Vigogo TASAC watimuliwa kikao cha Kamati ya Bunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imewatimua kwenye kikao vigogo wa Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC), kwa kushindwa kujibu hoja za ukaguzi ikiwamo bodi kufanya vikao vingi kinyume na sheria.

Akizungumza na Nipashe kuhusu mahojiano ya taarifa za hesabu za TASAC, mwenyekiti wa kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alisema katika hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), inaonyesha bodi hiyo ilitumia Sh. milioni 815 na katika vikao 13 vilivyofanyika.

"Lakini hawakuomba kibali "Sheria inaelekeza vikao vinatakiwa kuwa vinne kwa mwaka na vinaweza kuongezeka visivyo vya kawaida viwili hivyo kuwa jumla ya vikao sita na kama vikao vinazidi sita sheria inataka waombe kibali kutoka kwa msajili wa hazina."

"Kutoka kwa msajili wamefanya vikao 13 kwa mwaka huo na matumizi hayo wanalipana posho ya kikao na wanafanyia vikao nje ya ofisi na kuongeza gharama kubwa za uendeshaji," alisema.

Alisema hoja za CAG hazijatekelezwa na kila wakiulizwa maswali na wajumbe hawakuwa na majibu ya moja kwa moja.

"Majibu yaliyokuwa yakitolewa ni ya kubabaisha tumewatimua na wenyewe na tumewapa wiki mbili wakajipange walete majibu yanayoeleweka," alisema.

Alisema agizo jingine lilikuwa kuhusu urasimishaji wa bandari bubu ambalo halijatekelezwa.

"Mtendaji mkuu namna alivyokuwa anajibu anaonyesha haelewi mambo mengi maana hata kitu kisichomhusu mhasibu alikuwa anasema aulizwe mhasibu, hakuweza kujibu hoja, sasa mhasibu atajibu na ya kiutendaji, kwa mfano kwanini hawajahamia kwenye ofisi zao bado wamepangisha, eti Mtendaji Mkuu anasema aulizwe mhasibu, kamati ilijiuliza Mtendaji Mkuu anatosha?" Alihoji Kaboyoka. Naye, makamu mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema katika hoja za ukaguzi ilionyesha walipaswa kukusanya mapato Sh. bilioni 70 kwa mwaka, lakini walikuwa na madeni Sh. bilioni 38, zaidi ya nusu ya mapato yote zipo kwenye madeni hazijakusanywa na vitabu havijakaa vizuri.

"Pia, sheria inataka mashirika ya umma yachangie asilimia 15 ya mapato ghafi kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, sasa wao hawakuchangia kwasababu hawakukusanya mapato, kwa hiyo badala ya kuchangia zaidi ya Sh. bilioni 10, wakawa wamechangia Sh. bilioni nane na kufanya upungufu wa Shilingi bilioni mbili."

"Halafu sheria yao inawataka faida wanayoipata asilimia 70 ichukuliwe iende kwenye Mfuko Mkuu, ukiangalia katika asilimia 70 wao wamepeleka fedha kidogo sana, tumeona hawa wamevunja sheria na kanuni zilizowekwa na serikali na hivyo wanatakiwa wakajipange walete majibu kamili yanayostahili," alisema.

Kuhusu utoaji wa leseni, alisema: "Kisheria TASAC inatakiwa kutoa leseni kwa kila wakala anayeshughulika na masuala ya meli ikiwamo bandari, cha ajabu hadi sasa bandari hawajapewa leseni na TASAC na hawajaomba leseni ni tatizo kubwa."

Kuhusu mtaji, alisema inaonyesha zimeongezeka mchango wa Sh. bilioni 6.5, lakini kwenye vitabu inaonekana viwango tofauti na kumbukumbu zao hazijakaa vizuri.

"Pia wameshindwa kuwa na kanzidata ya kusajili meli zote, wakala zote na mifumo inayoonana mifumo ya bandari na serikali ambayo ingesaidia katika utendaji kazi wao suala ambalo limeonesha mashaka kuwa hawajajipanga sawa sawa na hawapo tayari kutekeleza majukumu ambayo wanaagizwa," alisema.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu fursa za kuwekeza katika viwanda vilivyobinafsishwa na kurejeshwa serikalini. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Udahili wa vyuo vikuu waongezeka

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imefungua awamu ya pili ya udahili wa shahada ya kwanza kwa mwaka wa masomo 2021/22, huku idadi ya waombaji kwa awamu ya kwanza ikiongezeka kwa wanafunzi 2,237.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema katika awamu ya kwanza ya udahili huo, waombaji 92,809 walituma maombi ya kujiunga na vyuo 74 vilivyoidhinishwa kudahili kulinganisha na waombaji 90,572 kwa mwaka uliopita.

Prof. Kihampa alisema programu 724 zimeruhusiwa kudahili ikilinganishwa na 686 zilizotumika mwaka 2020/21.

Alisema nafasi zilizopo mwaka huu ni 164,901 ikilinganishwa na 157,770 mwaka uliopita na kwamba hilo ni ongezeko la nafasi 7,131 sawa na asilimia 4.5 katika programu za shahada ya kwanza.

Prof. Kihampa alisema katika awamu ya kwanza ya udahili huo, waombaji 68,019 sawa na asilimia 73.2 ya waombaji wote wamepata udahili.

"Mwenendo wa udahili wa awamu ya kwanza kwa kipindi cha miaka minne unaonyesha ongezeko kubwa la waombaji, ikiashiria ongezeko la wahitimu wa kidato cha sita na wale wa stashahada.

"Idadi ya walioomba katika awamu ya kwanza ya udahili kwa kipindi cha miaka minne nayo imekuwa ikiongezeka," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Kihampa, waombaji waliodahiliwa katika zaidi ya chuo kimoja wanatakiwa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia leo hadi Septemba 6, mwaka huu, kwa namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili.

"Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri, ili kuthibitisha katika chuo husika.

"Na uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo mwombaji alitumia wakati wa kuomba udahili," alisema.

Pia alisema TCU imetoa nafasi ya udahili awamu ya pili, ili kutoa nafasi kwa wanafunzi wenye sifa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

## TANGAZO

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

# TANZIA



**AZARIA SIVONIKE**



**BENARD MUSHINGI**



**JOEL MITONDWA**



**FAHADI HAJI**



**SAIDI BUDDY**

Kwa niaba ya Menejimenti pamoja na watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa majonzi na masikitiko makubwa natoa taarifa ya vifo vya maofisa watano waliokuwa watumishi katika Idara ya Ushuru na Forodha vilivyotokana na ajali mbaya ya gari alfajiri ya tarehe **23 Agosti, 2021** eneo la **Hanseketwa**, **Old Vwawa** Wilaya ya **Mbozi** katika mkoa wa **Songwe**. Maofisa waliofariki ni;-

1. Bw. Benard Balagi Mushingi (40) Afisa Forodha (TRA-Songwe)
2. Bw. Azaria Asakwe Sivonike (42) Dereva (TRA-Mbeya)
3. Bw. Joel Isaya Mitondwa (36) Afisa Forodha (TRA- Mbeya)
4. Bw. Said Mrisho Buddy (34) Afisa Forodha (TRA- Mbeya )
5. Bw. Fahad Hassan Haji (26) Afisa Forodha Msaidizi (TRA- Mbeya)

TRA inatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na watumishi wa TRA kwa kuondokewa na wapendwa wetu ambao walikuwa siyo tu nguzo muhimu katika Mamlaka ya Mapato bali pia Taifa kwa ujumla.

Familia ya TRA itaendelea kuwakumbuka marehemu wote watano na kuenzi mchango wao katika kazi ya kukusanya mapato ya Serikali kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Sisi watumishi wenzao, vifo hivi vimetuacha na simanzi kubwa na pengo lisilozibika kirahisi kwa nguvu kazi tuliyoipoteza pamoja na kuzingatia maarifa na weledi waliokuwa nao.

Mwenyezi Mungu awape marehemu wote pumziko la amani na tunaombea familia zao Mungu aweze kuwapa nguvu za kuhimili mshtuko na pigo kubwa lililotokana na vifo hivi kwa vijana wetu.
Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina la Bwana lihimidiwe. Wapumzike kwa Amani. Amina

**A. J KIDATA**
**Kamishna Mkuu**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Motisha ya viwanja kwa walimu kuntu

**AGIZO** alilolitoa Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Thoba Nguvila la kutaka walimu ambao masomo yao yataongoza kiwilaya katika mitihani ya taifa ya darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita kupewa zawadi ya viwanja, ni muhimu likatekelezwa.

Kazi ya ualimu ni wito na inahitaji moyo wa kujitoa, kwanza kwa mazingira wanayopambana nayo kwa sasa kuanzia idadi ya wanafunzi wanaowafundisha kuzidi kiwango kinachotakiwa na ugumu wa maisha.

Ni kweli alichosema Mkuu wa Wilaya kwamba badala ya kuwaandikia barua za pongezi ni bora wapewe zawadi za viwanja kama motisha ya kuwapa ari ya kuendelea kufanya vizuri katika kazi yao.

Walimu wanapitia mazingira magumu, wengine wanaishi kwenye nyumba ambazo hazistahili kwa kazi yao wanayofanya.

Ualimu ni kazi inayotakiwa kupewa heshima ya hali ya juu kwa sababu wanaofanya kazi hiyo ndiyo wanaotoa marais, mawaziri, wabunge, wachumi na taaluma nyingine nyingi muhimu kwa taifa.

Pamoja na kufanya kazi nzuri, lakini walimu mara nyingi wanadharaulika hata na wanafunzi wanaowafundisha kutokana na maisha ya wanafunzi wao kuwa ni bora kuliko walimu wao.

Motisha za viwanja zitawawezesha angalau kudunduliza kwenye vipato vyao na kujenga nyumba nzuri zitakazowaletea heshima.

Mwalimu akiwa na kiwanja na kujenga nyumba ni kumbukumbu nzuri kwake na kwa familia yake kuwa alifanya kazi nzuri.

Walimu wengine wanapanga kwenye nyumba za wazazi wa wanafunzi wao kitendo ambacho kitamsababisha mwalimu wakati mwingine kutoa upendeleo kwa mtoto huyo ili akishindwa kulipa kodi asibugudhiwe na wazazi.

Mkuu huyo wa wilaya alitoa kauli hiyo wakati akikabidhiwa matangi ya kuvunia maji ya mvua, matundu 24 ya vyoo na vyumba vinne vya madarasa, vilivyojengwa na Shirika la World Vision Tanzania.

Nguvila aliahidi kutimiza azma hiyo ya kuwapa motisha ya viwanja walimu kwa mwaka huu kwa kutenga viwanja tisa kwa wale ambao masomo yao yatashika nafasi ya kwanza hadi ya tatu hatua ambayo itawafanya kuwa na ushindani katika ufundishaji.

Mbali na viwanja, wanaweza pia kupewa mikopo yenye riba nafuu itakayoweza kuwasaidia kufanya maendeleo yao badala ya kutegemea mishahara pekee.


Motisha nyingine wanazoweza kupewa, hasa kwa walimu wanaofanyakazi vijijini ambako miundombinu ya usafiri ni migumu ni kupewa vyombo vya usafiri kama pikipiki au baiskeli kuwarahisishia mwendo.

Baadhi ya walimu wanaikimbia kazi hiyo kwa kuchukizwa na mazingira na kutopata motisha ya kuwawezesha kuipenda kazi yao ili kutoa matokeo chanya kwa wanafunzi wao.

Kazi ya kufundisha wanafunzi zaidi ya 100 kwenye darasa moja inahitaji kuwa na uwezo wa kujitoa wa hali ya juu kwa kuwa kila mwanafunzi ana kiwango chake cha uelewa.

Agizo la Mkuu wa Wilaya liwe endelevu kuwapa moyo walimu wengi zaidi kufanya vizuri kwenye masomo yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mary Geofrey

# Hata wewe una nafasi kuitumia maabara hii

**MAMLAKA** ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), ina jukumu la kufanya uchunguzi wa sampuli zinazohusiana na makosa ya jinai ikiwamo ubakaji, ujambazi, kupatikana na viungo vya binadamu na mauaji kwa kutumia silaha za jadi na za moto.

Lakini inachunguza mauaji ya sumu, biashara na matumizi ya dawa za kulevya, wizi wa kutumia nguvu, ujangili, biashara na matumizi ya pombe haramu pamoja na masuala mengine yanayohusiana na hayo, anaeleza Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko.

Anafafanua kazi za mamlaka hiyo wakati anazindua Bodi ya GCLA, na kurejea mafanikio ya miaka minne iliyofanywa kuanzia 2018 hadi sasa na kueleza kuwa imechunguza sampuli 236,750 zinazosadikiwa kuwa ni dawa za kulevya.

Katika kutekeleza wajibu wake imechunguza sampuli 3,403 za matukio mbalimbali yanayohusiana na sumu, sampuli 3,913 za utambuzi wa makosa ya jinai yaliyohitaji uchunguzi wa kimaabara kwa kutumia teknolojia ya vinasaba vya binadamu na sampuli 3,332 zinazohusiana na makosa ya jinai juu ya ukiukaji wa taratibu za ubora.

Anawaambia wajumbe kuwa kundi la pili ni uchunguzi wa sampuli ili kubaini usalama na ubora wa bidhaa, ikiwamo mazao ya kilimo, ya uvuvi, mazingira, maji au maji taka na bidhaa za vyakula zinazozalishwa nchini na za nje.

Dk. Mafumiko anawaeleza wajumbe kuwa bidhaa nyingine zinazochunguzwa ni mbolea, ubora wa petroli, bidhaa na dawa za viwandani, dawa asili, kemikali na malighafi muhimu za kutengeneza bidhaa mbalimbali viwandani.

Anaendeleza kuwa katika katika kipindi cha miaka minne mamlaka ilichunguza sampuli 1,457 zinazohusina na usalama na ubora wa vyakula, sampuli 767 zinazohusiana na usalama na ubora wa dawa za viwandani na sampuli 319 zinazohusiana na ubora na usalama wa dawa asilia.

Anaeleza kuwa kundi la tatu linalochunguzwa ni sampuli zinazohusiana na masuala ya kijamii kama vile uhalali wa watoto, sampuli za utatuzi wa migogoro inayohusiana na mirathi na utambuzi wa miili iliyoharibika kutokana na majanga ya moto.

Anasema pia wanachunguza sampuli za ajali za meli, ndege, magari, kuangukiwa na majengo; kulipukiwa na bomu pamoja na kuzama majini.

Mkemia Mkuu anaeleza kuwa, katika kipindi hicho, mamlaka ilichunguza jumla ya sampuli za vinasaba vya binadamu 4,457 ili kubainisha uhalali wa watoto kwa wazazi na sampuli 153 za majanga ya ajali ili kutambua miili ya wahanga ikiwamo ajali ya lori la mafuta iliyotokea Msamvu mkoani Morogoro mwaka 2019 na kuua watu zaidi ya 100.

Mambo hayaishii hapo, Dk. Mafumiko anataja kundi la nne ambalo ni uchunguzi wa sampuli ili kupandikiza figo na utambuzi wa jinsi tawala na kwamba katika kipindi hicho, kwa kushirikiana na hospitali zinazotoa matibabu hayo ikiwamo Hospitali ya Taifa Mhimbili (MNH), ilichunguza jumla ya sampuli 48 ili kuwezesha matibabu ya upandikizaji wa figo.

Anasema pia walichunguza sampuli 22 ili kuwezesha matibabu ya utambuzi wa jinsi tawala kwa watu waliozaliwa na jinsi mbili.

Lakini anakumbusha kuwa inahusika na usimamizi wa sheria akisema kundi la tano ni kusimamia utekelezaji wa sheria tatu ambazo ni Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sheria Na. 8 ya 2016.

"Sheria hii pamoja na kuweka utu wa kisheria wa majukumu yote yanayofanywa na Mamlaka, inaongeza majukumu mengine mawili ya usimamizi na udhibiti wa maabara za kemia, sayansi jinai na vinasaba vya binadamu nchini ukiondoa maabara za tiba," anasema Dk. Mafumiko.

Umuhimu wa maabara ya serikali katika jamii ni mkubwa na hivyo ni jukumu la wananchi kufuatilia na kufahamu namna wanavyoweza kunufaika na huduma zinazotolewa.

Changamoto inayowaumiza watu inaweza isitatuliwe na ngazi za polisi lakini kwa kutumia GCLA, wakapata ufumbuzi, hivyo ni vyema kufuatilia na kufahamu zaidi kazi za makala hiyo ili Watanzania wa mijini na vijijini wanufaike.

# Samia kuhudhuria kuapishwa Hichilema

**Mwandishi Wetu na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajia kuondoka nchini leo kwenda nchini Zambia kuhudhuria sherehe za kuapishwa kwa Rais Mteule wa nchi hiyo, Haikande Hichilema.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, sherehe hizo zitafanyika katika Uwanja wa Taifa wa Mashujaa, jijini Lusaka.

Rais Samia ataambatana na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka.

Wengine ni Katibu wa Idara ya Oganaizesheni wa CCM, Maudline Cyrus Castico, Waziri Mkuu mstaafu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Mizengo Pinda, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Kombo Hassan Juma.

Wengine ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Henry Shekifu, na Mbunge wa Mtera na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Livingstone Lusinde.

Pia Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, atashiriki sherehe hizo akiwa ni kiongozi wa timu ya waangalizi wa uchaguzi mwaka huo, kutoka Jumuiya ya Madola.

Hichilema (59) wa Chama cha UPND aliibuka mshindi kwenye uchaguzi uliofanyika Agosti 12, mwaka huu, akiwa na kura milioni 2.8 na kufuatiwa na Edgar Lungu wa Chama cha PF ambaye alikuwa rais tangu mwaka 2016 aliyepata kura milioni 1.8.

Wakati huo huo, uongozi wa Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha Viziwi Tanzania (KISUVITA), umempa tuzo Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kutambua mchango wake katika kuhakikisha haki na usawa wa fursa kwa watu wenye ulemavu nchini.

Walisema wanamtambua Rais Samia pia kutokana na kuwawezesha kufanikiwa kushiriki mashindano ya kidunia ya mitindo na urembo Moscow nchini Urusi.

Tuzo hiyo imewasilishwa na kupokelewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka kwa niaba ya Rais Samia.



Mafundi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), wakihamisha nguzo za umeme ili kupisha ujenzi unaoendelea wa barabara katika eneo la Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Mabibo mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Meya Manispaa ya Shinyanga afariki kwa ugonjwa wa moyo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA**.**

MEYA wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, na Diwani wa Ndembezi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), amefariki dunia kutokana na ugonjwa wa moyo.

Nkulila amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga.

Msemaji wa familia, Mary Joseph, alisema jana kuwa kifo cha meya huyo, kilitokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa 11:00 alfajiri.

Alisema Nkulila alikuwa akisumbuliwa na tatizo la moyo kwa muda mrefu na mara kwa mara alikuwa akilazwa hospitalini kupatiwa matibabu na kuruhusiwa, lakini siku za hivi karibuni hali yake ilianza kuwa mbaya zaidi na hatimaye kufariki dunia.

"Marehemu ni mjomba wangu na kifo chake ni pigo kubwa katika familia yetu. Ameacha watoto wanne na mazishi yake yatafanyika siku ya Jumatano (kesho) hapa hapa mjini Shinyanga katika Makaburi ya Dodoma," alisema Joseph.

Naibu Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Ester Makune, alisema kifo hicho kimemshtua kwa sababu walikuwa na mipango mizuri ya kuiletea maendeleo manispaa hiyo na kuipeleka kuwa hadhi ya jiji.

Naye Diwani wa Kambarage, Hassan Mwendapole, alisema kiongozi huyo alikuwa mtu mwenye maono, shupavu, mpenda maendeleo, mzalendo, mchapakazi, mwenye misimamo na malengo.

Katibu wa CCM Kata ya Ndembezi, Pendo Sawa, alisema kifo cha meya huyo ni pigo ndani ya chama kwa sababu alikuwa msema kweli na mtekelezaji wa ilani ya CCM kwa vitendo.


WOMEN FUND TANZANIA TRUST
Empowering Local Women Heroes

THE REGISTERED TRUSTEES OF WOMEN FUND TANZANIA

TANZIA



ZUKIVAH NJALAI MIHYO

SEPTEMBA 28, 1952 – AGOSTI 20, 2021

Kwa masikitiko makubwa, Bodi ya Udhamini wa Mfuko wa Wanawake Tanzania, Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust), Uongozi, Wafanyakazi, na kwa niaba ya wanamtandao wenzetu, tunatoa taarifa ya msiba wa Mkurugenzi mwenzetu, rafiki na mwanaharakati mpendwa dada yetu, Zukivah Njalai Mihyo. Dada Zuki alikuwa kati ya waanzilishi wa WFT mwaka 2011, na hatimaye akawa mmoja wa wanachama na Mkurugenzi wa WFT Trust hadi mauti yalipomkuta tarehe 20 Agosti 2021.

Dada Zuki alikuwa mtaalamu na mtafiti mbobezi wa haki za wanawake, usawa wa kijinsia, na maendeleo ya kijamii. Tunaposherehekea maisha ya mpendwa wetu Dada Zuki, tunaenzi na kutambua alivyokuwa akijituma na kujitolea kwa kiwango kisichopimika ili kuendeleza harakati za usawa wa kijinsia nchini Tanzania na kwingineko.

Women Fund Tanzania Trust inashukuru na kutambua na kuenzi juhudi zake katika kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika kipindi chote cha uhai wake. Daima tutaenzi mchango wake mkubwa kwenye upanuzi wa programu za WFT Trust katika kutoa ruzuku zilizoweza kuwafikia wanawake na wasichana wengi wenye uhitaji katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania.

Vilevile, Women Fund Tanzania Trust, tunaungana na wanaharakati watetezi wa haki za wanawake hapa Tanzania na nchi za kanda ya Kusini Mwa Afrika (SADC) kuenzi, kutambua, na kuthamini mchango wa mpendwa wetu Dada Zuki katika kuchagiza utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na kikanda inayohusu haki za wanawake na usawa wa kijinsia ikiwemo Azimio la Beijing na lile la usawa wa kijinsia katika kanda ya Kusini mwa Afrika (SADC). Dada Zuki atakumbukwa kwa kuendeleza jitihada za uzingatiaji wa misingi ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake katika sera, michakato ya maendeleo, pamoja na kujenga uwezo wa taasisi na makundi mbalimbali kuhimiza utekelezaji na ufuatiliaji wa matokeo. Dada Zuki alitoa mchango mkubwa katika kuboresha tafiti zenye mrengo wa kijinsia ili kuwezesha utungaji wa sera na mipango iliyojikita kwenye takwimu sahihi na ushahidi wa hali halisi ya haki za wanawake na usawa wa kijinsia katika maeneo mbalimbali. Pia, Dada Zuki alishiriki kwenye utetezi katika ngazi za kisera na maamuzi ikiwemo uratibu wa awali wa jukwaa la kisera kuhusu usawa wa kijinsia na haki za wanawawake lijulikanalo kama Gender Mainstreaming Working Group-Macro Policy.

Tunapoungana na familia yake kuomboleza kifo cha mpendwa wetu Dada Zuki, pamoja na kusherehekea safari ya maisha ya mwenzetu tutaendelea kuenzi na kukumbuka uongozi wake thabiti, ubunifu, na uwezo wake mkubwa wa kujenga mahusiano na kufuatilia fursa mbalimbali ili kuendeleza haki za wanawake na usawa wa kijinsia nchini Tanzania na kwengineko.

Daima tutakumbuka tabasamu lake mwanana, moyo wa utajiri, furaha iliyojaa ari, na utu wake wa kipekee. Roho yake ya upendo na ucheshi utaendelea kuwa chanzo cha nguvu na matumaini yetu siku zote.

**Tunaiombea Roho Yake kupumzika katika Amani ya Milele.**

**Wasiliana Nasi:**
**SLP 72935 Dar Es Salaam Tanzania.**
**info@wftrust.or.tz**
**WomenFund_TZ**
**Wft.tz**
**www.wft.or.tz**

HABARI KITAIFA

# Makumbusho ya Taifa Dar yaibua fursa kupitia ubunifu

**Na Ally Mlanzi,** TUDARCO

MAKUMBUSHO ya Taifa Dar es Salaam, imeandaa programu maalum ya kuonyesha vijana fursa mbalimbali zilizopo kwenye sekta ya utalii na utamaduni.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Idara ya Programu ya Makumbusho ya Taifa, Chance Ezekiel, wakati wa mahojiano na Nipashe kuhusu mwamko wa vijana kutembelea vivutio vilivyopo.

Alisema Makumbusho hiyo imekuja na ubunifu wa kuandaa makongamano na matamasha ambayo yanawakutanisha wenye vipaji na ubunifu mbalimbali kama uchoraji, utunzi wa vitabu, vikundi vya ngoma za asili na sarakasi.

Alisema wameandaa programu mbalimbali kama vile 'Twenzetu Makumbusho' 'Kazi Sanaa' na 'Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni' ambazo zinawakutanisha vijana wenye vipaji mbalimbali waliopo vyuoni na mtaani, ili kuwaonyesha fursa zilizopo kwenye sekta ya utalii na utamaduni.

Alisema, "Sisi lengo letu ni kuwaonyesha vijana fursa zilizoko kwenye sekta ya utamaduni, ili waweze kujiajiri na kuacha kutegemea kuajiriwa."

Aidha, alisema kwa sasa mwamko wa vijana wa kutembelea Makumbusho umekuwa mkubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma na kwamba sababu kubwa ni ubunifu.

Pendo Anthony, ni moja ya vijana wanufaika wa matamasha hayo, alisema yalimsaidia kujuana na watu mbalimbali ikiwamo kumwezesha kubadili mtazamo kwenye ubunifu.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariyam Mwinyi, akizungumza wakati wa ufunguzi wa tamasha la Kizimkazi, ambapo lilianza kwa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wa Mkoa wa Kusini Unguja katika Shule ya Kizimkazi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wafugaji nyuki wahimizwa kujiunga ushirika

**Na Costantino Michael,** TUDARCO

WAFUGAJI wa nyuki wametakiwa kujiunga kwenye vyama vya ushirika, ili kufikiwa na elimu na fursa mbalimbali za masoko ya mazao ya asali ndani na nje ya nchi.

Kamishna Msaidizi anayesimamia rasilimali za nyuki kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Hussein Msuya, alisema jana kuwa, licha ya kutoa elimu kwa wafugaji kutambua umuhimu wa kijiunga kwenye ushirika bado mwitiko ni mdogo.

"Ushirika unasaidia kuweka nguvu ya pamoja katika kuongeza tija kwenye sekta ya asali kuliko uzalishaji wa mtu mmoja mmoja. Lakini bado tunaona mwitikio ni mdogo jambo linalosababisha wafugaji wengi kutokupata taarifa ya masoko ya asali na elimu ya kuzingatia ubora kwenye uzalishaji,"alisema Msuya.

Pia alisema wameanza utaratibu wa kufufua vyama vya ushirika na kuvipa nguvu vinavyolegalega ili kufikia soko la kimataifa na kwamba ni lazima wafugaji wazalishe kwa tija kwa kuongeza uzalishaji wa asali isiyokuwa na mabaki ya kemikali inayohitajika kwa sasa kwenye soko la dunia.

"Changamoto kubwa tuliyo nayo ni wafugaji wengi hawana elimu ya ufugaji kwa tija, uhifadhi na ufungashaji wa asali. Kwa kutambua hilo, tumeendelea kuwafikia wafugaji kwenye vikundi vyao na kuwafundisha namna bora ya uzalishaji wa asali inayokidhi vigezo vya soko la kimataifa," alisema.

Msuya alisema katika soko la asali la kimataifa kuna aina mbili za asali zinazohitajika ambazo ni asali ya mezani (table honey) na asali ya viwandani (industry honey) na kwamba nchini uzalishaji wa asali hizo tunatumia mapori ya akiba na hifadhi za misitu.

Alisema katika maeneo hayo hakuna shughuli za kibinadamu na uzingatiaji wa njia sahihi pamoja na uwapo wa mazingira ya asili na udhibiti wa mabaki ya kemikali katika asali jambo linalofanya asali ya Tanzania kukubalika soko la kimataifa.

# Watoto 700 kunufaika na taulo za kike

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHILINGI milioni 18.4 zinatarajiwa kutumika kununua taulo za kike kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na misaada kwenye vituo vinne vya watoto yatima mjini Kibaha.

Misaada hiyo kutoka Shirika la SOS la Marekani, inatarajia kutolewa kati ya kesho hadi Agosti 29, wakati wa sherehe ya Ishara na Maajabu itakayofanyika stendi ya zamani ya Maili Moja, mjini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana, Mchungaji Water Zuniga kutoka Sweden, alisema sherehe hizo zinalenga kutoa ujumbe wa upendo kwa madhehebu yote ya dini.

Zuniga ambaye anamwakilisha mwasisi wa sherehe hizo, Amriza Johanes, alisema watoto wa kike 500 hadi 700 watanufaika na taulo hizo huku vituo vya watoto yatima vikipatiwa magodoro na mablaketi.

Aidha, alisema wapo madaktari ambao watakuwa wanatoa huduma za upimaji ikiwamo wa macho katika maeneo mbalimbali ya mitaa ya Kibaha.

Mwenyekiti wa Makanisa ya Kipentekosti Mkoa wa Pwani, Askofu Uswege Mwakisyala, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika sherehe hizo kwa kuwa wagonjwa wataombewa na kupona.

"Acheni kuwapeleka wagonjwa na watu wenye matatizo sugu kwa waganga wa kienyeji. Waleteni watafunguliwa siku hizi tano za sherehe ya Ishara na Maajabu," alisema.

Mwakisyala alisema kamati ya amani ya mkoa huo imeshirikishwa kuhusiana na sherehe hiyo na kwamba kila mmoja bila kujali madhehebu, ataombewa na kufunguliwa matatizo yake.

Sherehe hizo zimeshafanyika kwenye nchi 25 mataifa 40 na kwa miaka saba zimekuwa zikifanyika kwenye mikoa tofauti hapa nchini.

**Zuniga ambaye anamwakilisha mwasisi wa sherehe hizo, Amriza Johanes, alisema watoto wa kike 500 hadi 700 watanufaika na taulo hizo huku vituo vya watoto yatima vikipatiwa magodoro na mablaketi.**

## Serikali yaombwa kuweka vifaa kuwakinga wenye ulemavu corona

**Na Sabato Kasika**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeombwa kuweka vifaa vya kunawia mikono kwenye stendi za mabasi, kwa ajili ya kujikinga na corona, vinavyozingatia mahitaji ya abiria wenye ulemavu.

Ombi hilo limetolewa juzi na Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), baada ya kubaini kutokuwapo kwa vifaa vya maji tiririka ambavyo ni rafiki kwa watu hao.

Msemaji wa CHAKUA, Solomon Nkiggi, alisema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili na kufafanua kuwa serikali imejitahidi kuweka vifaa hivyo kila stendi kubwa, lakini vingine wenye ulemavu hawawezi kuvitumia.

"Kwa mfano, pipa la maji linawekwa juu ya ngazi maalum, kwa mwenye ulemavu anayetambaa hawezi kulifikia, hivyo tunaomba Wizara ya Afya kuangalia uwezekano wa kuweka vifaa kwa ajili ya makundi yote," alisema Nkiggi.

Alisema, CHAKUA ina maofisa wasimamizi wake karibu mikoa yote ambao hutoa elimu kwa abiria ya kujikinga na corona na wameshuhudia kukosekana kwa miundombinu rafiki ya vifaa hivyo kwa ajili ya wenye ulemavu.

"Serikali imejitahidi kuhakikisha inawakinga wananchi wake dhidi ya corona, kwa kuweka huduma zote katika stendi kuu za mabasi, lakini Arusha kuna changamoto ya kutokuwapo kwa vifaa vya kunawia mkono vinavyozingatia mahitaji ya abiria wenye ulemavu," alisema.

Pia alisema, baadhi ya vifaa vya kunawia si rafiki kwa watu hao kwa kuwa hawawezi kuvifikia kutokana na ulemavu wao.

"CHAKUA imesambaza maofisa wasimamizi karibu mikoa yote ambao wanatoa elimu kwa abiria ya kujikinga na ugonjwa, na wanaijua hali halisi ambayo baadhi ya wenye ulemavu wamekuwa wakimbana nayo," alisema.

Alisema, wao kama wadau wa usafiri wamejitosa kushirikiana na serikali kutoa elimu kulingana na mwongozo wa kudhibiti corona, uliotolewa hivi karibuni na Wizara ya Afya, ambao unazuia mabasi kujaza abiria kupita kiasi.

"Tunaunga mkono serikali katika kupambana na corona kwa kutoa elimu na kuelekeza pia wamiliki wa mabasi kuhakikisha abiria na wahudumu wote wanavaa barakoa na kutumia vitakasa mikono kabla ya kupanda," alisema.

Nkiggi alisema, katika harakati hizo wamebaini hali hiyo ambayo wanaishauri miumdombinu iwe rafiki kwa kila mtu anayefika stendi kwa ajili kutafuta usafiri au kusindikiza.

"CHAKUA kama wadau wa usafiri, tunaipongeza serikali kwa juhudi inazofanya kuhakikisha wananchi wakiwamo abiria wanakuwa salama, na tunashauri juhudi hizo ziheshimiwe," alisema.

# Sendiga aipa polisi siku 5 upelelezi kesi za ubakaji

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ametoa siku tano kwa Jeshi la Polisi mkoani Iringa kukamilisha upelelezi wa kesi za ubakaji na ulawiti ndani ya mkoa huo na watuhumiwa wote wafikishwe mahakamani.

Sendiga alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Ingingilanyi, Wilaya ya Iringa baada ya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika halmashauri ya wilaya hiyo.

Alisema hataki kuona kesi za ulawiti na ubakaji watuhumiwa wakiendelea kuachwa bila kufikishwa mahakamani kwa kuwa ucheleweshaji huo ni chanzo cha kuongezeka kwa matukio hayo.

Aliliagiza jeshi hilo upelelezi wa kesi zote za ubakaji na ulawiti zilizofikishwa katika vituo vyote vya polisi zinafanyiwa kazi haraka ili wahusika wachukuliwe hatua stahiki.

"Nataka kuona kesi zote za ubakaji na ulawiti watuhumiwa wake wanafikishwa mahakamani na sheria ipo wazi, ubakaji na ulawiti ni miaka 30 niwatake wananchi wanaojihusisha na vitendo vya ukatili kama huu kutambua wazi kuwa wakifikishwa mbele ya vyombo vya sheria adhabu ipo wazi bora tu ushahidi ukamilike," alisema.

Alisema polisi wanapopokea watuhumiwa wa ubakaji na ulawiti wanapaswa kuelekeza nguvu zao zote kukamilisha upelelezi wa kesi hizo ili wahusika kufikishwa mahakamani kwa wakati.

Alisema matukio ya ukatili wa kijinsia ndani ya mkoa wa Iringa ni mkubwa na hayapendezi kuendelea kusikika ndani ya mkoa huo.

"Nilipofika mkoani Iringa kuanza kazi nilikuta kuna tatizo la udumavu kwa asilimia 47, lakini pamoja na tatizo hilo bado nilikuta matukio ya ukatili wa kijinsia kuwa juu, sasa najiuliza kama mkoa unatatizo la udumavu hivi nguvu za kubaka na kufanya ukatili kwa wanawake na watoto linatoka wapi...nasema siwezi kuvumilia polisi nawaagiza chukueni hatua kali," alisisitiza.

Pia, alipiga marufuku unywaji pombe muda wa kazi na kuagiza wenyeviti wa serikali za vijiji na vitongoji kuhakikisha sheria za vileo zinafanyiwa kazi kwa maeneo ya kuuza pombe kufunguliwa kwa muda uliopangwa kuanzia saa 10 jioni.

Kuhusu tatizo la maji, aliagiza mamlaka zinazohusika na maji kuharakisha utekelezaji wa miradi na kwenye maeneo yenye kero kufika na kutatua.

Alisema lengo la serikali ni kuona tatizo la maji linashughulikiwa kwa haraka zaidi ili kumwepusha mama kufuata maji umbali mrefu.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuendelea kuchukua tahadhari ya janga la corona kwa kuvaa barakoa na kupata chanjo.

Moyo aliwataka wananchi kuepukana na upotoshaji unaofanywa na watu wachache kuhusu chanjo na kuwa suala la afya ya mtu ni la mtu mwenyewe.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Jumuiya ya CCM, Dk. Philis Nyimbi, akizungumza na viongozi wa umoja huo wa Mkoa wa Dar es Salaam juzi, kuhusu masuala mbalimbali ya UWT. Kushoto ni Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa huo, Florance Masunga na Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC), Angel Akilimali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rukwa yapaa makusanyo ya mapato

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKOA wa Rukwa umefanikiwa kukusanya mapato kutoka Sh. bilioni 14.56 katika mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia Sh. bilioni 19.7 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, aliyasema hayo jana wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020/2025 katika kikao kilichofanyika mjini hapa.

Alisema katika kipindi cha mwezi Novemba 2020 hadi Juni, 2021 makusanyo ya mapato (kodi za ndani na kodi za forodha na ushuru wa mauzo), yalikuwa Sh. 13,820,795,466.73 kati ya lengo la Sh. 10,579,130,000.00.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Rukwa, ilikusanya Sh. 19,709,923,276.47 kati ya lengo la kukusanya Sh. 15,393,550,000.00.

Alisema takwimu hizo ni mafanikio ya ongezeko la makusanyo halisi ya mapato kutoka Sh. 14,563,041,782.30 mwaka 2019/2020 hadi Sh. 19,709,923,276.47 kwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la Sh. 5,146,881,494.17.

Alisema katika kipindi hicho TRA ilizidi kusimamia matumizi ya mashine za EFD kwa kuhakikisha kila mfanyabiashara anayekidhi vigezo amenunua mashine na kuendesha mazoezi maalum ya kuhamasisha utoaji wa risiti za kielektroniki na kuwahimiza wananchi kudai risiti kwa kila ununuzi wanaofanya.

Pia katika mwaka wa fedha 2020/2021, halmashauri zilikisia kukusanya Sh. 9,487,289,000.00 kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021, halmashauri zimekusanya Sh. 8,428,477,428.27 sawa na asilimia 88.84 ya makisio ya mwaka.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Rukwa, Rainer Lukalah, aliipongeza serikali ya mkoa katika jitihada za kukusanya mapato pamoja na kuyasimamia vizuri hatua itakayo iwezesha serikali kutekeleza miradi ya maendeleo na kuwaondolea kero zinazo wakabili wakazi wa mkoa huo.

HABARI KITAIFA

# Wenye ulemavu waomba elimu chanjo UVIKO-19

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKISHO la Chama cha Watu wenye Ulemavu mkoani Shinyanga (SHIVYAWATA), limelalamikia kutopatiwa elimu dhidi ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, pamoja na chanjo ya UVIKO -19.

Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Richard Mpongo, alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema watu wenye ulemavu wapo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi ya virusi vya corona au kueneza, kutokana na kuhitaji msaada hasa wenye uoni hafifu, kwa kushikwa mikono na kuvushwa kwenda mahali pengine na kwamba wakipatiwa elimu na kuchanjwa itawasaidia kujikinga na ugonjwa huo.

"Watu wenye ulemavu tumesahauliwa kupewa elimu ya kujikinga na janga hili la virusi vya corona pamoja na chanjo, na sisi ni kundi ambalo lipo katika hatari kubwa ya kuambukizwa au kueneza, tunaiomba serikali itupatie elimu hii ya corona," alisema Mpongo.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Tanzania wilayani Shinyanga (TLB), Michael Petrol, alisema kumekuwapo na upotoshaji mkubwa dhidi ya chanjo ya corona na kusababisha kuingia hofu kupata chanjo hiyo, na kwamba wakipata wataalamu wa afya wa kuwapatia elimu sahihi wapo tayari kupata chanjo hiyo.

Vile vile, alisema serikali imewasahau na kushindwa kuchapisha vitabu vya nukta nundu vinavyotoa elimu ya corona na kuwasambazia ili wavisome na kupata ufahamu zaidi wa kujikinga na virusi hivyo badala ya kusikia kupitia kwa watu ambao siyo wataalam wa afya na kuwapotosha.

Mratibu wa chanjo mkoani Shinyanga, Timoth Sosoma, alisema wameshaanza kutoa elimu ya corona na chanjo kwa makundi hayo maalum kwa kuanza na wazee kambi ya Kolandoto, na kubainisha watapanga ratiba kutoa elimu kwa watu hao.




Vijana wakivunja zege ili wapate chuma chakavu, katika eneo la Ilala jijini Dar es Salaam jana kwa ajili ya kwenda kuuza ili wajipatie ujira wa siku. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mrema awashangaa wanaopinga chanjo corona

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Tanzania Labour (TLP), Augustino Mrema, amewataka wananchi kuwapuuza baadhi ya watu wakiwamo wanasiasa wanaopinga chanjo ya corona, akidai kila mtu anawajibika kwa afya yake.

Aidha, amesema kuchanja ni sawa na polisi anapokwambia funga mkanda unapokuwa kwenye gari, anakusaidia ili ukipata ajali usipate madhara zaidi.

Akizungumza jana katika mahojiano nyumbani kwake Sinza jijini Dar es Salaam, alisema kuendelea kuwasikiliza wanaopinga chanjo hiyo ni kupoteza muda, kwani kila mtu anatakiwa kujali afya yake mwenyewe.

Alisema ameshapata chanjo na hawezi huchezea afya yake. Alihoji kuwa watu wote wakiugua corona, mitungi ya gesi ya oksijeni utapatikana wapi na kwamba watafia majumbani.

Mrema alisema siyo mara ya kwanza kwa wananchi wa Tanzania kupata chanjo, lakini inashangaza chanjo hii ya corona imekuwa na upinzani mkali sana, na cha kushangaza miongoni mwa wanaopinga ni viongozi wa kisiasa.

"Kuchanja sawa na polisi anapokwambia funga mkanda unapokuwa kwenye gari, anakusaidia ili hata ukipata ajali huwezi kuumia sana, kwa sababu mkanda utakuzuia," alisema Mrema.

Mrema alisema hofu kwamba waliochanjwa baada ya muda watakuwa mazombi, hizo ni kauli za kuwatia hofu kwani wataalamu waliobobea wa masuala ya afya wameshathibitisha kuwa chanjo hiyo ni salama.

Alisema hakuna sababu ya kuingiwa na hofu katika suala hili, kwani bahati nzuri hata Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha njia kwa kupata chanjo hiyo, ambayo inaendelea kutolewa katika nchi mbalimbali duniani.

Baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiikosoa chanjo hiyo, hivyo kuibua malumbano na baadhi ya viongozi wa serikali.

Mpaka Agosti 14, mwaka huu idadi ya wanaume waliochanjwa ni asilimia 58.3 sawa na 121,002 na 86,389 ni wanawake sawa na asilimia 41.7.

# Wakulima waomba mapitio mfumo Bodi ya Pamba

**Na Happy Severine,** BARIADI

WAKULIMA wa pamba wilayani Bariadi, mkoani Simiyu, wamemwomba Mbunge wa jimbo hilo, Andrew Kundo, kufanya marejeo na mapitio ya mifumo inayotumiwa na Bodi ya Pamba katika ukataji wa fedha na ugawaji wa pembejeo za kilimo.

Kadhalika, wamemwomba kuwasaidia kufufua ama kuunda upya chama cha wakulima wa zao hilo ili wapate chombo cha kuwasemea matatizo yao badala ya kulazimishwa kujiunga na vyama vya ushirika (Amcos) ambavyo wamesema haviwasaidii na badala yake vinawakandamiza na kuwanyonya.

Wakulima hao walitoa kilio hicho jana wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na mbunge wao katika Kata ya Mhango, halmashauri ya wilaya hiyo.

Mmoja wa wananchi hao, Charles Mwita, alisema kuna kero ndani ya bodi ya pamba hususani katika mfuko wa pembejeo kwa kuwa mfuko huo unawakata wakulima fedha za pembejeo, lakini wakulima hawapati mbegu. Mwita alisema tatizo la mbegu limekuwapo kila mwaka pamoja na viuatilifu na kumwomba mbunge wao kuangalia upya mfumo ambao bodi ya pamba imekuwa ikitumia katika kugawa pembejeo hizo.

"Wakulima sisi tumekuwa na wakati mgumu sana...wakati wa kwenda kuuza pamba yetu tunakatwa fedha kibao ikiwamo ya mbegu na viuatilifu, lakini bado mbegu hizo hatuzipati za kutosha na wakati muafaka," alisema.

Baada ya kusikiliza kero hizo, mbunge huyo alisema kuwa tatizo hilo limekuwapo muda mrefu na kwamba kuna uzembe wa baadhi ya viongozi wa juu ngazi ya wilaya wa kutofuatilia wala kutatua kero hiyo na baadhi yao wameonekana kunufaika na utaratibu huo.

"Haiwezekani ndani ya wilaya tukawa na watu wanaowachezea wakulima na kwa haraka nimegundua kuwa tatizo haliko kwa Amcos wala wasambazaji wa pembejeo hizo bali lipo kwa viongozi wa wilaya," alisema Kundo.

Pia, alisema analichukua suala hilo na atawasiliana na wataalamu wa wizara hiyo kufanya uchambuzi wa mifumo hiyo ili iweze kupitiwa upya na kuboresha sekta ya kilimo.

"Nimekutana na malalamiko mengi sana juu ya usambazaji wa mbolea, mbegu na viuatilifu, nitaomba wizara kupitia upya mifumo hiyo, hasa kwenye zao la pamba ambalo wakulima wengi wamekuwa wakilalamika," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, David Masanja, alisema wakulima wamekuwa wakichezewa michezo mibaya, lakini ifikie wakati michezo hiyo iwe basi.

Alisema kwa kushirikiana na mbunge wake watasimamia na kutatua tatizo hilo hivyo wakulima waondoe shaka kila kitu kitaenda sawasawa.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 24, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Wilaya inavyoibuka kimikakati kwenye sayansi, yaandaa wasomi sekondari**



Ukurasa 12

Mabinti wanapompata mlezi mbadala kuzikabili mimba, utoro



Ukurasa 13

Kasi kubwa ya UVIKO-19 ni maswali zaidi ya majibu

SAYANSI

**NA ADELA MADYANE, KIGOMA**

# Baadhi ya 'zawadi' anazopata mtoto unapomsafirisha ili akatumikishwe

• Ulemavu, sonona, majeraha na makovu



Watoto wakitumikishwa kuchimba na kuchenjua dhahabu kwa sumu ya zebaki. **PICHA: MTANDAO**

WAZAZI na walezi wanaweza kuwa chanzo cha kukwamisha maendeleo ya watoto kielimu na kimaisha, kutokana na kuruhusu watumikishwe kwenye ajira ngumu wakati walitakiwa kuwa darasani kujifunza.

Watoto wanasafirishwa kutoka vijijini hadi mijini kufanyakazi za ndani, kutunza mifugo, mashamba au bustani, ili ujira wanaolipwa utumiwe kutunza familia zao zilizokobakia nyumbani.

Ndiyo sababu Ofisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo wilayani Kakonko mkoa wa Kigoma, Mohammed Shauri, anakemea mazoea hayo na kuwataka wazazi na walezi kuacha kuwageuza watoto kuwa wakombozi wa familia kwa kuwatuma kwenda kufanya shughuli za kujiingizia kipato mijini, ambako hawajui wanachokumbana nacho.

Anaonya: "Wanaposafirishwa mbali kufanya kazi, ili kuzisaidia familia zao kiuchumi, wanakutana na ukatili unaowapotezea haki na utu wao na kusababisha waishi maisha magumu zaidi yenye mateso kama kupigwa na kunyimwa chakula. Wengine wanatumikishwa mchana na usiku, kuishi kwa simanzi na hata kupata ulemavu kutokana na mateso. Wapo wanaopata mimba ututoni, wengine kunanajisiwa kingono, pia kutukanwa muda wote."

Katika mahojiano na Nipashe, anasema watoto wanaosafirishwa kufanya kazi ni wadogo wenye umri wa kati ya miaka 10 hadi 17, ambao wanatakiwa kuwa darasani na utumikishwaji huo unaharibu ndoto zao, tena ni kinyume cha sheria.

Akizungumzia kusafirisha watoto kwenda mikoani kutumikishwa, Mkurugenzi wa Jukwaa la Utu wa Mtoto Kigoma, Koshima Mtengati, anasema usafirishwaji huo, unasababisha ukatili kama ukatili wa kingono unaowaathiri kisaikolojia.

"Watoto wa umri wa kusoma ni lazima waende shule, watawasaidia wazazi zaidi watakupokuwa na kazi baada ya kuhitimu masomo yao, kuwatumikisha sasa hakuwasaidii wazazi na walezi, lakini zaidi inaongeza mnyonyoroo wa umaskini katika familia," anaeleza

### VISA VYA UKATILI

Mtengeti anasema matukio yaliyoripotiwa kwa watoto nchini mwaka 2019 na 2020 yanaonyesha kuwa kuna kazi ya kufanya, anasema kuanzia 2015 mpaka 2019 kesi 36,940 za ubakaji, unajasi kinyume na maumbile kwa watoto zimeripotowa katika vituo vya polisi nchi nzima, na kwa mwaka 2020, kesi za aina hiyo 45 zimefikishwa mahakamani kutoka mikoa 13 ya Bara ambapo 13 kati ya hizo zilitolewa hukumu.

Aidha ripoti ya Jeshi la Polisi, inaonyesha ongezeko la asilimia 25.95 la ukatili dhidi ya watoto. Katika mwaka 2020 ambapo visa 7,388 viliripotiwa kote nchini tofauti na mwaka 2015, matukio yalikuwa 5,803.

Ripoti hiyo inataja miongoni mwa ukatili dhidi ya watoto ulioripotiwa kwa kiwango kikubwa ni unyanyasaji kingono, hii ikiwa ni sawa na visa 615 kwa mwezi jambo ambalo linatajwa kuwa linahatarisha mustakabali wa ustawi kwa watoto nchini kielimu.

### ATHARI SERA YA ELIMU

Pamoja na juhudi za serikali kugharamia elimu, ili kuhakikisha watoto wanakwenda shule, bado wanaacha masomo kutokana na sababu mbalimbali.

Takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) huonyesha ongezeko la watoto wanaoacha shule, zinasema jumla ya watoto 167,834 waliacha masomo katika shule mbalimbali za msingi mwaka 2019 ikilinganishwa na 66,142 walioacha 2017.

Zinabainisha ongezeko la zaidi ya mara mbili ya uwiano wa wanafunzi walioacha shule walioandikishwa shule za msingi. Ongezeko hilo ni kutoka asilimia 0.7 hadi asilimia 1.6 katika kipindi hicho.

Takwimu zinaendelea kueleza kuwa watoto wa kiume wanaoacha shule wameongezeka hadi asilimia 58 ya watoto wote ukilinganisha na asilimia 55 kati ya mwaka 2017 na 2019.

Zinaendelea kueleza kuwa watoto 96,683 wa kiume waliacha shule mwaka 2020 Ikilinganisha na wa kike 71,151.

Aidha, mwaka 2017 walikuwa wavulana 36,434 na wasichana 29,708 na kwamba takribani nusu ya wanafunzi wote walioacha masomo walikuwa darasa la tatu na nne. Katika mwaka huo, wanafunzi 52,684 wa darasa la nne waliacha masomo, huku 42,765 wakiwa wa darasa la tatu kwa mwaka 2019.

Mikoa iliyoongoza kwa watoto kuacha shule ni Geita, kwa idadi ya wanafunzi 21,969 Simiyu 19,496, Kagera inafuata ikiwa na wanafunzi 17,274 walioacha shule, Tabora 15,566 na Mwanza 13,845, huku Mkoa wa Kigoma ukiwa na watoto 9,887.

INAENDELEA UK.13

SAYANSI

**NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA**

# Mabinti Pwani wanapompata mlezi mbadala kuzikabili mimba, utoro



Wanafunzi wanaoshiriki mradi wa Room to Read wakijadili mambo mbalimbali ya kufanikisha masomo yao. **PICHA: JULIET MKIRERI**

KUWA karibu na binti na kushiriki makuzi yake ni moja ya mambo yanayomsaidia kuepuka matatizo kama mimba za utotoni na kumlinda dhidi ya vishawishi vingi ndani ya jamii.

Licha ya kwamba kukaa karibu na binti na kumsaidia ni jukumu la mama na mlezi, baadhi ya wadau wamejitosa kushirikiana nao, ili kuwapa wasichana elimu ya malezi na makuzi wakiwa shuleni.

Shirika la Room to Read (RR) ni moja ya asasi hizo, ambazo linafanya kazi kwa kushirikiana na jamii pamoja na serikali kutekeleza mradi wa usawa wa kijinsia na elimu kwa msichana katika shule za msingi na sekondari zilizopo Mkoa wa Pwani.

Meneja Mwandamizi wa Mradi wa Usawa wa Kjinsia na Elimu kwa Wasichana wa shirika hilo Zamaradi Said, anasema lengo ni kuwawezesha wasichana kumaliza elimu ya sekondari na kuwapatia ujuzi muhimu zikiwamo elimu ya stadi za maisha na ushauri zinazojumuisha umuhimu wa elimu ya makuzi.

Zamaradi anaiambia Nipashe kuwa, mradi huo umejikita kuwafunza stadi za maisha katika shule za msingi kuanzia darasa la tano hadi la saba wakati sekondari ni kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

> “Kupitia miradi wanayoitekeleza kumekuwa na mabadiliko chanya ya kitabia kwa wasichana na kukua kwa kiwango cha ushiriki wa wazazi katika masuala ya elimu.

“Tunapoanza kutekeleza mradi wetu kwenye shule tunaisaidia shule kwa miaka mitano, baada ya hapo inaendelea yenyewe na stadi za maisha kwa madarasa ya vijana wanaojiunga baada mradi kuhamia katika maeneo mengine. Tulianza kazi hii mwaka 2012,” anasema

Mkoani Pwani wanafanya kazi katika Wilaya za Kibaha Mji, Chalinze na Bagamoyo wakijikita kutoa elimu ya stadi za maisha, fedha na ujasiriamali, ushauri, msaada wa vifaa na ushirikishwaji wa familia, shule na jamii, anasema Zamaradi.

### LENGO LA MRADI

Anasema ni wasichana kuendelea kusoma hadi wafikie malengo yao, huku wakiwa na stadi muhimu za maisha zitakazowanufaisha hata baada ya shule.

“Suala la mimba ni tatizo ambalo tumekabiliana na tunaendelea kulikabili tunaamini kwamba wasichana wanahitaji stadi, maarifa na taarifa sahihi kuhusu afya ya uzazi na makuzi na wanahitaji kabla hawajapata ujauzito, ili wasiangukie kwenye tatizo hilo,” anaeleza meneja huyo.

Anasema kupitia elimu hiyo wamepata mafanikio mengi ikiwa ni pamoja na kukuza kiwango cha ufaulu kwa wasichana katika mitihani ya ndani ya shule na ile ya kitaifa kwa darasa la saba, kidato cha pili na cha nne .

“Mfano tathmini zetu zinaonyesha kuwa maeneo tunayofanya kazi tumepunguza idadi ya wasichana wanaoanguka na kuacha shule kutoka asilimia 18 mwaka 2014 hadi asilimia 0.5 mwaka 2020, mdondoko huu pia umehusisha sababu ya ujauzito” anabainisha.

Zamaradi anasema mafunzo ya stadi za maisha na ushauri yamewafikia walimu zaidi ya 30 katika shule za mradi na kuwajengea uwezo wa kutekeleza stadi za maisha na ushauri shuleni hata pale mradi unapohamia katika maeneo mengine.

Anasema kupitia miradi wanayoitekeleza kumekuwa na mabadiliko chanya ya kitabia kwa wasichana na kukua kwa kiwango cha ushiriki wa wazazi katika masuala ya elimu.

Anasema hata hivyo, wanatambua kwamba zaidi ya wasichana 6,500 nchini huacha shule kila mwaka kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito, kundi ambalo ni kubwa likiachwa litazorotesha maendeleo ya nchi kiuchumi na jamii.

“Tunashirikiana kuimarisha jitihada za kuwawezesha wasichana walioacha shule kupata elimu, stadi na maarifa na hivyo kujiunga na mfumo rasmi wa elimu na kuendelea kufikia ndoto zao, tutaendeleza juhudi za kuzuia mdondoko, ili kupunguza au kumaliza kabisa kikwazo cha wasichana kuacha shule,” anaelezea.

June 15 mwaka huu, RR ilizindua mradi wa Stadi za Maisha, Elimu ya Fedha na Ujasiriamali (Nguvu ya Msichana Project) ukilenga sekondari wilayani Chalinze.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Maendeleo iliyopo Kibaha Mjini, Mariam, Mkama anasema miradi ya shirika hilo, imeleta mafanikio hususani kupunguza utoro.

Mariam anasema wanafunzi hao wamepatiwa elimu ya kujisimamia na kuanzisha miradi ambayo inawasaidia kujikwamua na hali duni kwenye familia zao.

"Asilimia kubwa ya wanafunzi katika shule yangu wanaishi na bibi zao, wengine wanalelewa na mama bila baba hii inasababisha kuwapo na kesi za kupelekana polisi kwa sababu za utoro na wengine kwa ujauzito , huku baadhi wakisema wanashindwa kununua vifaa vya shule kutokana na hali duni ya maisha," anasema Mariam.

Anasema kwa mwaka 2020 shule hiyo imekuwa ya pili katika Wilaya ya Kibaha na hakuna msichana aliyefeli, pia kwasasa hakuna kesi za kupelekana polisi kwa utoro au mimba.

"Nimekuwa mkuu wa shule kwa miaka 15 sasa, lakini katika shule hii tangu nimeletwa hapa kulikua na kesi za utoro kutokana na hali duni za maisha kushindwa kununua vifaa vya shule na mimba kwasasa hakuna tatizo kama hilo elimu ya kujisimamia imewasaidia" anasema Mwalimu Mkuu.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa hivi karibuni mwaka 2020 wanafunzi zaidi ya 130 walikatisha masomo kutokana na mimba shuleni, kati yao shule za msingi ni 39 na sekondari ni zaidi ya 100.

SAYANSI

**NA MICHAEL ENEZA**



Mmoja wa viongozi wa dini akipatiwa chanjo ya Johnson &Johnson jijini Dar es Salaam, baada ya kuzinduliwa rasmi mwezi uliopita. **PICHA: MTANDAO**

# Kasi kubwa ya UVIKO-19 ni maswali zaidi ya majibu

## • Inavyolazimisha chanjo ya ziada

HALI ya hewa ya matumaini ya kuzuia UVIKO-19 kwa matumizi ya chanjo ya corona, imechukua sura nyingine baada ya tafakuri ya kina kwanini maambukizi yamekuwa yakiongezeka kutokana na wimbi la aina ya delta, kirusi chenye kasi kubwa zaidi ya maambukizi. Wakati baadhi ya watafiti walianza kusema inaonyesha chanjo si jibu kwani hata waliopata wamekuwa wakiambukizwa, ila kwa uchache zaidi na mara nyingi hawapati madhara makubwa, lipo jawabu tofauti. Ni kudungwa nusu dozi ya ziada baadaye.

Mwanzo wa mwezi huu ilitangazwa kuwa Israel imekuwa nchi ya kwanza kuanza kusambaza dozi ya tatu kwa sababu nusu dozi, mwanzoni mtu alikuwa akidungwa mara mbili kupata dozi nzima , sasa ni mara moja. Kuanza kwa maelekezo hayo kumechukua sura ya tahadhari kama ilivyokuwa mwanzoni, kuwa wanaohitaji chanjo ya ziada au dozi ya tatu kwa lugha ya vyombo vya habari, hasa ni wale wenye umri zaidi ya miaka 60. Lakini maelekezo haya inaelekea yatakuwa ya muda mfupi, kwani pale mwanzoni ilidhaniwa ni kundi la walioko umri wa tatu au wazee, ndiyo watahitaji chanjo sasa vijana nao wanachanjwa.

Kuna upande mwingine wa suala hilo kuwa kupewa chanzo zaidi ya moja, kuwa hadi sasa ni chanjo ya Pfizer/ BioNTechl ambayo imo katika kuongeza chanjo, hali ambayo inaweza kutokana na kuwa wengi zaidi walitumia chanjo hiyo mwanzoni. Chanjo ya Moderna ilikuja baadaye na hii ya Johnson&Johnson ilikuwa na matatizo kadhaa wakati inapitishwa na kwa sababu hiyo ilikuwa rahisi zaidi kwa serikali ya Marekani kuipatia Tanzania chanjo hiyo kwani unaweza kusema kuwa zilikuwa hazitoki sana, kutokana na kinachoonekana ni hitilafu kwa watu wenye matatizo ya moyo, shinikizo la damu. Matumizi yake hapa nchini hata hivyo yanaonyesha kuwa hitilafu hizo zinahitaji dawa za kawaida kama 'diazepam' na si za kuleta kihoro.

Wakati utawala wa Israel ulikuwa tayari umeanza kampeni ya kutoa chanjo ya tatu hasa kwa wazee, Marekani ilikuwa inatafakari bado, na kuna wakati Shirika la Afya Duniani (WHO) liliingilia mjadala huo kusema kuwa nchi zinazoendelea zipelekewe chanjo za kutosha kwanza. Lilipaza sauti kusema kuwa siyo sawa au haki kwa nchi zilizoendelea kujilundikia chanjo na kuanza kutoa dozi mara ya tatu, wakati mamilioni ya watu nchi zaidi ya 90 duniani ikiwamo Afrika hazijaanza kutoa chanjo kwa wote wanaostahili au wanaotaka.

Ni msimamo uliosikika hivi karibuni katika mkutano wa wakuu wa nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambako mwenyekiti wake mpya, Rais Lazarus Chakwera wa Malawi, alitaka nchi za Afrika zipewe teknolojia ya kutengeneza chanjo, kwani ni haki ya wote kuokokoa maisha yao na kukingwa na maradhi.

Taarifa za awali za kutolewa kwa chanjo hiyo ya ziada zinaonyesha kuna ufaulu katika kuzuia maambukizi na kujengeka kwa ugonjwa mwilini endapo mtu amekutana na maambukizi ya kirusi cha delta. Hata hivyo, hizo ni taarifa za awali tu kwani Marekani na nchi za Ulaya hazikuweza kukubaliana umuhimu wa kuchanjwa dozi inayoitwa ya uimarishaji wa chanjo ya awali kwa haraka katika majadiliano mwezi uliopita. Ni suala ambalo halijaanza kujadiliwa katika nchi nyingi, kwani hata ile chanjo ya awali, bado.

Katika hatua hizi za mwanzo za kujenga hoja ya kudungwa sindano ya tatu (kwani mfumo unaotumika aina nyingine za chanjo ni kudungwa mara mbili, kuacha hii ya Johson&Johnson) ni Israel ambayo imeongoza katika suala hilo. Sababu ni kuwa iliweka mifumo ya kijeshi ya kudunga sindano za chanjo ya Pfizer/ BioNTech mapema wakati nchi nyingine zinatafakari matumizi yake. Ila kwa sehemu kubwa njia ambayo Israel imepitia Marekani haichukui muda kuelekea huko huko, kwani inakuwa ndiyo kithibitisho kuwa dozi hiyo ya ziada

> Juni, mwaka huu, nchini Ufaransa, Wizara ya Afya ilisema kuwa asilimia 20 ya wagonjwa wa COVID-19 nchini humo, walipatikana na kirusi kipya cha delta.

inapunguza maambukizi na kushusha kiwango kikubwa cha kasi ya maambukizi hasa ya wimbi hili la kirusi cha delta. Ni kama vile Israel ni maabara; ikifaulu kutoa majibu Marekani inafuata.

Mwanzoni mwa wiki hii, mtaalamu mwandamizi wa tassisi kuu ya magonjwa ya kuambukiza, Anthony Fauci, ambaye ndiye mshauri wa Ikulu ya Marekani kwa sera kuhusu corona, alisema kuwa Marekani iko tayari kwenda haraka zaidi katika suala la kutoa chanjo ya ziada. Hata hivyo daktari bingwa mmojawapo katika taasisi ya Bina ya Afya ya nchi hiyo alikuwa akiondoa uwekezako wa kutolewa kwa chanjo ya tatu kwa walio na umri mkubwa.

Baadaye wataalamu wengine wamekuwa wakieleza kuwa hospitali kadhaa zimeanza kutoa chanjo ya ziada kwa watu wenye upungufu wa kinga, ambayo inajumlisha umri mkubwa na magonjwa sugu yasiyoambuliza, kama moyo, shinikizo, kisukari na figo..

## Baadhi ya 'zawadi' anazopata mtoto unapomsafirisha ili akatumikishwe

**INATOKA UK.11**

**WADAU WATAKA UELEWA**

Seleman Abdul, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyangwe wilayani Kigoma, anasema uelewa wa mzazi na mlezi kwenye umuhimu wa elimu una mchango mkubwa kwenye maendeleo ya motto.

Lakini, anasema kumekuwa na tofauti kwani hujali zaidi elimu ya msingi kuliko kuwapeleka sekondari, wengi huona umuhimu wa kuwasomesha watoto ngazi ya msingi, ila baada ya kuhitimu hutamani kuwaagiza wakafanye kazi za ndani hasa kwa watoto wa kike na biashara kwa wanaume.

Anasema hata ikitokea mtoto amefaulu kwenda sekondari wazazi hutafuta sababu, ili asiendelee na masomo.

Mkurugenzi wa shirika la Wote Sawa la mjini Kasulu, Jacqueline Ngalo, anasema wanapowapokea watoto walioathirika na ukatili unaosababishwa na usafirishwaji,watoto wenye umri wa kurudi shule hufanyiwa taratibu za kujrudishwa shule, na ambao umri umepita huingizwa katika elimu ya ujasiriamali.

"Mbali na watoto kusafirishwa kwa ajili ya kufanya kazi za kujiingizia kipato, zipo sababu nyingine zinazowafanya kuacha shule ambazo ni pamoja na ufugaji, biashara ndogondogo na migogoro ya kifamilia," anafafanua Jacqueline.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Wilaya inavyoibuka kimikakati kwenye sayansi, yaandaa wasomi

YANAPOTAJWA masomo ya sayansi, juhudi mbalimbali zinafanyika ikiwa ni pamoja na kujenga sekondari maalumu za kila mkoa za wasichana, ili taifa liwe na hazina ya akiba ya wanawake wanasayansi, shule hizo zinaanza kuandaliwa mwaka huu.

Masomo hayo yanapigiwa chapuo na wadau wa elimu, ili kuwahamasisha wanafunzi wayapende na taifa kuwa na wataalamu wengi wa baadaye wa fani hiyo watakaoshughulikia mahitaji na changamoto mbalimbali za nchi.

Katika harakati za kuhakikisha lengo hilo linatimia, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, imeanza mkakati wa kuzigeuza baadhi ya sekondari zake kuwa za kidato cha tano na sita zitakazofundisha masomo ya sayansi. utekelezaji wa mkakati huo, ukianza mwakani, kama Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya, Majidu Karugendo, anavyoieleza Nipashe hivi karibuni.

Anazitaja sekondari hizo kuwa ni ya Rusoli, Kiriba, Mugango na Bugwema ambazo anafafanua kuwa zina maabara za masomo yote matatu ya sayansi ambayo ni kemia, fizikia na baiolojia.

"Wilaya ya Musoma ina sekondari 21 na nyingine zinaendelea kujengwa, lakini tutaanza na nne, ili nasi tutoe wataalamu wa fani mbalimbali watakaowezesha taifa kusonga mbele " anasema Karugendo.

Anaeleza kuwa kinachoendelea katika sekondari hizo ni walimu kuwahamasisha wanafunzi, ili kupenda masomo ya sayansi pia kuwafundisha kwa vitendo kwa kutumia maabara zilizopo shuleni.

"Ni muhimu kuandaa vijana wetu wakati huu ambao nchi inaelekea kwenye mabadiliko ya viwanda, nasi tunataka wataalam wa fani mbalimbali watokee huku kwetu, siyo maeneo mengine tu," anasema.

Ofisa Elimu Karugendo anawaomba wadau wa maendeleo ya elimu kuendelea na moyo wa kuchangia uboreshaji wa miundombinu ya sekondari, ili kuhakikisha shule zote zinakuwa na maabara tatu na maktaba.

Anatolea mfano Mugango Sekondari, kwamba ina maabara zote tatu zinafanya kazi, lakini inakabiliwa na uhaba wa baadhi ya miundombinu mengine ambayo anaona ni muhimu kushirikisha wadau kuiboresha.

Akizungumzia maboresho ya miundombinu hiyo, Mkuu wa shule hiyo, Chacha Ragita, anaelezea uhaba huo na kusema ni wa madarasa 20 wakati yaliyoko ni 16 pekee wakati idadi ya wanafunzi ni 800.

Shule ina uhaba wa nyumba za walimu ziko nne, wakati zinazohitajika ni 18 na kuongeza kuwa kuna walimu 18, lakini mahitaji halisi ni 25.

"Tunaamini serikali itaongeza wengine kadri inavyowezekana, pia kwenye vyoo, kuna matundu 24, yanayohitajika ni 34, hivyo tunawaomba wadau wasichoke kusaidia kuboresha mindombinu ya shule hii," anasema Ragita.


Aidha, anasema, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilishatoa vifaa vya maabara zote tatu na pia kuchangia Shilingi milioni 75, kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike ambao mkuu huyo wa shule anafafanua kuwa tayari umeanza.

" Pia mbunge wa jimbo, Profesa Muhongo ametoa mifuko 130 ya saruji na vitabu mbalimbali vikiwamo vya masomo ya sayansi zaidi ya 2,000, kwa ajili ya maktaba ya shule yetu ni sehemu ya fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo," anasema.

Anaongeza kuwa shirika la Water Aids Tanzania nalo limetoa matangi mawili ya maji yenye ukubwa wa lita 5,000 kila moja kwa ajili ya matumizi ya shule na kwenye maabara.

Aidha, Ragita, anazungumzia ufaulu, akisema kwa upande wa ufaulu wa mitihani kidato cha nne mwaka 2020 , watahiniwa walikuwa 83, huku waliofaulu daraja la kwanza wakiwa wanne, daraja la pili watano, daraja la tatu 14, daraja la nne 39 na daraja la sifuri 21.

"Kwa upande wa matokeo ya kidato cha pili, watahiniwa walikuwa 175, ambapo daraja la kwanza walikuwa nane, daraja la pili 11, daraja la tatu19, daraja la nne 121 na daraja la sifuri 16," anasema.



Baadhi ya wanafunzi wakijifunza masomo ya sayansi kwa vitendo, katika moja ya maabara ya shule hiyo. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICHA WETU**

> Ni muhimu kuandaa vijana wetu wakati huu ambao nchi inaelekea kwenye mabadiliko ya viwanda, nasi tunataka wataalam wa fani mbalimbali watokee huku kwetu, siyo maeneo mengine tu.



Wanafunzi wakijisomea nje ya madarasa.

**UHAMASISHAJI**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Charles Magoma, anasema madiwani na viongozi wengine akiwamo mbunge, wanashiriki kukamilifu kuhamasisha wananchi kuchangia shughuli za maendeleo ya elimu.

Magoma anasema, uhamasishaji huo umeingia kuifanya halmashauri hiyo kuwa na sekondari 21 ambazo wananchi wameshiriki kwa hali na mali kuzijenga ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu.

"Wananchi wamekuwa wakitoa nguvukazi ya kusomba, maji, mawe, mchanga na kokoto na wakati mwingine kuchangia fedha, ili kuunga mkono serikali katika ujenzi wa sekondari katika maeneo yao," anasema Magoma.

Mwenyekiti huyo anasema, hatua inayofuata sasa ni kuhakikisha halmashauri hiyo inakuwa na shule japo nne za kidato cha tano hadi cha sita za masomo ya sayansi, ili kuwa na wataalum wengi wa baadaye.

"Tunatamani wanafunzi wa mchepuo wa sayansi wanaofaulu kidato cha nne katika mikoa mingine waje waendelee na masomo yao katika sekondari zetu, ili nasi tutoe wataalam," anasema.

Halikadhalika, anasema wanaunga mkono juhudi za kuleta mapinduzi ya kiuchumi, ili kuibadili Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

"Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa ambao sasa unaingia awamu ya tatu unatarajiwa kufanikishwa na uwapo wa rasilimali watu wakiwamo wataalamu wa sayansi na teknolojia," anasema.

Anasema dira hiyo inalenga kutayarisha idadi ya kutosha ya Watanzania walioelimika na kupenda kujielimisha zaidi, ili kulifanya taifa lipate maendeleo na kuwa lenye uchumi wa kati na shindani ifikapo mwaka 2025 ambayo ni miaka minne kuanzia sasa.





# Ndugai ahimiza kambi mitihani ya taifa

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kusimamia na kufuatilia kila shule iwe na kambi kwa madarasa yenye mitihani ya taifa ili kukuza kiwango cha ufaulu.

Ndugai alisema hayo katika mkutano wa Baraza la Madiwani wa kupitia taarifa za Mamlaka ya Mji Mdogo Kongwa na Kibaigwa kwa kipindi cha robo ya nne ya mwaka uliofanyika mwishoni mwa wiki wilayani humo.

Alisema suala la kambi kwa madarasa yenye mitihani ya taifa ni muhimu, hivyo madiwani wanapaswa kuwa mstari wa mbele kulisimamia hilo ili wanafunzi wapate kiwango kizuri cha ufaulu.

"Nawaomba madiwani mliangalie hilo. Tunahitaji kuona kiwango cha ufaulu kinaongezeka," alisema Spika Ndugai.

Kuhusu kilimo, Ndugai alisema halmashauri inapaswa kuweka kipaumbele kwa mazao ya alizeti, zabibu na korosho kwa kutafuta mbegu bora na kuhamasisha wananchi kulima kwa wingi kwa kuwa yana tija kwa biashara na kukuza uchumi wa nchi.

Ndugai pia alisisitiza wananchi kupata hati za maeneo yao ili kuwapa umiliki halali.

Katika hatua nyingine, Ndugai alikemea suala la madalali katika masoko ya mifugo kwa kuwa linawanyonya wafugaji na kumtaka Mkuu wa Wilaya ya Kongwa kuwaondoa mara moja.

Sambamba na hayo, Ndugai ambaye ni Mbunge wa Kongwa, alisisitiza wananchi kuchanja chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na ugonjwa wa corona.

"Mtu asiyechanja ana matatizo gani? Acheni kusikiliza mitandao ya kijamii, mtaacha familia zenu bure, kachanjeni jamani," alisema Ndugai.

Alisema neno hiari kwa mtu mzima ni kumpima aone umuhimu wa hilo jambo yeye mwenyewe kwa hiyo wananchi wakachanje.

Spika huyo aliwahamasisha wananchi kujitokeza na kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa kuwa kwa sasa Wilaya ya Kongwa inakabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa 107 kwenye shule za sekondari.

Naye Mkuu wa Wilaya hiyo, Remidius Emmanuel, alisema kutokana na upungufu wa madarasa, atazindua kampeni ya kufyatua matofali 100,000 kila kijiji ambayo yatatumika kujenga vyumba vitano vya madarasa.

Pia aliwataka waratibu wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kufuatilia matumizi ya fedha zinazochukuliwa na wananchi kama zinafanya kazi za maendeleo.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika (BOA), Wasia Mushi, akifungua warsha ya mafunzo ya kibiashara kwa wateja wa biashara za kati wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka miundombinu rafiki kwa wenye ulemavu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WALIMU wenye ulemavu nchini, wameiomba serikali kuboresha miundombinu ya shule zilizojengwa miaka ya nyuma ambazo hazina miundombinu rafiki kwa ajili yao.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kwenye kongamano la walimu hao, Mwalimu wa Shule ya Msingi Mtundu mkoani Kagera, Ng'ombe Shimozirana, alisema shule zilizojengwa zamani hazina miundombinu rafiki kwao na kusababisha kuongeza ulemavu kutokana na kuanguka mara kwa mara.

Pia alisema vyoo wanavyotumia wanalazimika kushika chini kwa mikono kutokana na wengine kutambaa, hivyo kuiomba serikali kulipa kipaumbele suala hilo ili kuwaepusha na magonjwa mbalimbali.

"Unakuta shule imejengwa na ngazi msingi unakuta mita mbili, na sisi tunaotumia magongo au viungo bandia ukitumia nguvu gongo linavunjika na kujisababishia maumivu au ulemavu mwingine," alisema Shimozirana.

Aliomba Ofisi ya Waziri Mkuu kitengo kinachoshughulikia watu wenye ulemavu, kuliangalia suala hilo kwa umakini ili kuwaongezea ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema kuna baadhi ya shule ambazo zinajengwa hivi sasa zimewekewa miundombinu hiyo lakini za zamani hazina.

Naye Mwalimu Aloyce Masero kutoka mkoani Mwanza, alisema: "Wenye ulemavu wanaotumia mikono na jamii ya kawaida wanatumia choo aina moja kwa hiyo suala hili ni hatarishi kwa walimu hao kupata magonjwa kwa sababu kushika sehemu chafu kupitia mikono yao."

Kadhalika, alisema suala la viungo bandia vimekuwa bei ghari mno jambo linalosababisha wengi kushindwa kumudu kununua kutokana na kipato chao kuwa duni.

"Unakuta mguu wa bandia unauza Sh. milioni moja au zaidi. Ukiangalia mshahara wako haufikii huko, hivyo tunaomba serikali itusaidie hilo ili kumudu hizo gharama," alisema Maselo.

Kuhusu walimu wasioona ambao wanakuwa na wasaidizi wa kuwaongoza, aliomba serikali kuwasaidia kupata posho za wasaidizi hao ili kuwasaidia walimu kwa moyo.

Maselo alisema wasaidizi hao ni muhimu sana kwa wasaidizi hao kupata posho kwa sababu hao ndio huwaongoza njia walimu wenye ulemavu ili kufika katika vituo vyao vya kazi.

Alisema wanahitaji kutoa elimu bora kwa wanafunzi hivyo serikali iangalie suala zima la kuboresha miundombinu ya shule pamoja na kulipa posho za wasaidizi wa walimu wenye ulemavu wa macho.

# Wadau waombwa kusaidia waishio mazingira magumu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WADAU wa mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali wameombwa kuendelea kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ili wajikwamue na umaskini.

Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, alitoa ombi hilo jana jijini hapa alipokuwa akifunga mkutano wa tathmini ya Mradi wa Kizazi Kipya ambao umefanya kazi kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2016 na utakoma Septemba, mwaka huu.

"Naomba tuendeleze mradi. Walipotufikisha tuendelee mbele, ikiwamo halmashauri na wadau wetu, niwaombe tunayoyafanya haya tuyafanye kwa moyo mmoja. Tuendelee kuzifanya kazi hizi ni za kujitolea," alisema Chibago.

Naye Meneja wa Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto wa Shirika la World Vision, Daudi Gambo, alisema wadau, serikali na jamii kwa ujumla wanatakiwa kuendelea kushirikiana ili kuhakikisha wanaikomboa jamii kutoka kwenye umaskini.

"Tushikane mikono tutaendelea, pamoja tutaenda mbali World Vision itaendelea kufanya kazi, mmejengewa uwezo msimame imara," alisema Gambo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Action for Community Care (ACC), Pendo Maiseli, alisema mradi wa Kizazi Kipya umejikita kwenye vipaumbele vinne.

Alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni afya, elimu, kuinua vipato vya kaya pamoja na ulinzi na usalama.

"Mradi huu umewanufaisha vijana waliotoka katika mazingira magumu kwa kuwapatia ujuzi wa kufanya kazi, watoto kutoka kaya maskini wamenufaika kwa kupelekwa shule na kupatiwa mahitaji ya kielimu," alisema.

Mmoja wa wanufaika, Frank Mlewa, alisema kuwa mradi huo umemsaidia kupata ujuzi wa ufundi kwa kuwa wamesomeshwa katika chuo cha ufundi (VETA).

"Mradi umenikuta nikiwa mtaani, tulikuwa wengi ulitukusanya ukatuunganisha pamoja ukatupa elimu katika chuo cha ufundi na sasa ni fundi. Naweza kujitegemea na nimepanga kwa sasa najitegemea," alisema Mlewa.

Alisema watoto, vijana na walezi takribani 16,000 wamenufaika katika mradi huo uliotekelezwa na Shirika la ACC na KISEDET.



# Mtoto anayedaiwa kubakwa na baba yake amliza mama kortini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, ililazimika kuahirisha kusikiliza kesi ya jinai inayomkabili baba (jina limehifadhiwa) fundi seremala mkazi wa Pambogo, jijini hapo anayetuhumiwa kumwingilia na kumbaka mtoto wake wa kumzaa mwenye umri wa miaka minne, baada ya ushahidi wa mtoto huyo kumliza mama yake kortini.

Mahakama hiyo ilianza kumsikiliza mama mzazi wa mtoto anayedaiwa kuingiliwa ambaye ni mwanafunzi wa chekechea katika shule moja jijini Mbeya.

Ijumaa iliyopita, mtoto huyo akihojiwa na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, wakili Davice Msanga, aliiambia mahakama kuwa baba yake ndiye aliyemwingilia sehemu za siri mbele na nyuma baada ya kumwonyesha kwa kidole mbele ya mahakama hiyo.

Huku akionekana mwenye kuogopa anapotajwa baba yake mzazi, mtoto huyo ameonyesha kwa vidole sehemu ambazo aliingiliwa na baba huyo.

Hata hivyo, wakati akihojiwa na baba yake kipindi cha maswali na majibu, mtoto huyo alisikika akimwambia baba yake huyo kuwa aliyemwingilia ni mtu mwingine ambaye ni mtoto mwenzake. Lakini alipohojiwa tena na wakili wa serikali alisisitiza kuwa aliyemfanyia kitendo hicho ni baba yake.

Baada ya kauli ya mtoto huyo, mama wa mtoto alishindwa kuvumilia na kuangua kilio mbele ya mahakama hiyo kwa awamu mbili tofauti.

Mama mzazi wa mtoto huyo jina (limehifadhiwa), alidai hajaolewa na baba huyo, lakini wamezaa mtoto mmoja ambaye ni mwathirika wa tukio hilo.

Alidai kwa sasa anaishi Iringa ambako anasoma na anafanya kazi kama ofisa mikopo kwenye kampuni moja.

Alisema wakati wa likizo mwanawe aliwasiliana naye ili aende kumsalimia na baada ya kufika Juni 16, mwaka huu, huko Iringa akiwa anamwogesha ndipo mtoto huyo alisikika akilalamika kuwa anaumia sehemu za siri na kurudia kauli hiyo siku inayofuata hatua iliyomshtua na kuamua kumchunguza na kuongea naye ili kujua amefanya nini.

Alidai baada ya kumhoji alimwambia ameingiliwa na mtoto aliyemtaja (jina linahifadhiwa) na aliamua kupeleka taarifa polisi na baadaye hospitalini kwa ajili ya matibabu na uchunguzi wa kitabibu.

Vile vile, alidai kuwa daktari katika Hospitali ya Frelimo Iringa, alisema mtoto huyo aliingiliwa na mtu mzima na sio mtoto mwenzake na ndio maana amechubuka kwenye baadhi ya maeneo ya sehemu za siri za mwili wake.

Mama huyo aliiomba mahakama kutenda haki kwa ajili ya mwanawe ambaye aliingiliwa na kubakwa na ametoa picha mbili ambazo alimpiga sehemu za siri baada ya kufanyiwa kitendo hicho.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Davice Msanga, aliiomba mahakama kuahirisha kesi hiyo na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, aliahirisha kesi hiyo.

Mtuhumiwa anashtakiwa kwa tuhuma za kumbaka mwanawe mwenye umri wa miaka minne na miezi nane na kumsababishia maumivu.




Maofisa wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, wakichukua taarifa muhimu za gari la abiria linalofanya safari zake kati ya Mji wa Mbalizi na Nsalaga, baada ya kupata ajali katika eneo la Njia Panda ya Itende, jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Homera aunda timu kuchunguza matumizi mil. 500/-

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameunda kamati ya watu watano kuchunguza matumizi ya Sh. milioni 500 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuanza ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela, baada ya kutoridhishwa na matumizi ya fedha hizo.

Alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea mradi wa ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika hospitali hiyo na kushuhudia fedha zote milioni 500 zikitumika kujenga msingi pekee wa jengo hilo.

Alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, kutoa maelezo ya kina ya namna alivyotokeleza mradi huo.

Mkurugenzi Magehema alimweleza, Homera kuwa kiasi hicho cha fedha kilitumika kujenga msingi wa jengo hilo alilodai kuwa kutokana na ujenzi ulivyokuwa fedha zote Sh. milioni 500 zilitumika kwa msingi huo pekee.

Alisema kuwa msingi huo wenye kimo cha futi mbili kutoka chini hadi juu, umesukwa kwa nondo nyingi, mawe na matofali ambayo yamegharimu kiasi kikubwa cha fedha.

Kwa upande wake Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Mosha Mwamtobe, alisema halmashauri hiyo imeshapokea jumla ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa wodi hiyo.

Akifafanua, Mwakatobe alisema walipokea awamu ya kwanza Sh. milioni 500 ambazo walizitumia kununua vifaa vya ujenzi, kulipa mafundi na kuanza ujenzi wa msingi wa jengo hilo.

Alisema katika hatua ya awali Sh. milioni 460 zilitumika na baadaye serikali ikawapatia Sh. milioni 500 nyingine ambazo hazijatumika na mpaka sasa zipo benki kwenye akaunti ya hospitali hiyo.

"Kwa fedha ambazo zililetwa na serikali tumeshatumia Sh. milioni 460 na mpaka sasa bado tuna fedha zaidi ya Sh. milioni 540 ambazo zipo benki," alisema Mwakatobe.

Alisema wapo wadau wa maendeleo ambao pia walichangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi hiyo wakiwamo benki za NMB na CRDB ambao kwa ujumla wao walitoa Sh. milioni 50 ambazo pia zimeshatumika katika ujenzi wa wodi hiyo.

Baada ya maelezo hayo, Homera alionyesha kutoridhishwa na matumizi ya fedha hizo na ndipo akachukua uamuzi wa kuunda timu kuchunguza suala hilo.

# Serikali yaandaa mpango matumizi bora ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi, imeanza kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kwenye vijiji 20 katika kata 14 za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa lengo la kuwezesha wananchi kumilikishwa ardhi kwa mujibu wa sheria.

Utaratibu huo unadaiwa utasaidia kupunguza migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara na wakati mwingine kuhatarisha hali ya amani kwenye kata hizo.

Kabla ya mpango huo, maofisa wa Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi, wameanza kutoa elimu kwa wananchi wameanzia katika Kata ya Igale ambayo ni miongoni mwa kata zinazonufaika.

Meneja wa Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Pili Msali, alisema kwenye utekelezaji wa mradi huo wameshapokea vijana 30 kutoka katika Chuo cha Ardhi kilichoko mkoani Dar es Salaam.

Alisema kati ya vijana hao, 24 ni wataalamu wa Mipango Miji na Vijiji na sita ni wapimaji ambao wote wameelekezwa katika kata hizo 14 za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambao watagawanywa kwenye vijiji 20 ambavyo vipo kwenye mpango.

"Tunataka tutoke na mpango wa makazi bora kwenye vijiji vitano, mpango wa matumizi bora ya ardhi na zoezi hili litafanyika kwa muda wa siku 30, tarafa zote za halmashauri hii zitaguswa," alisema Pili.

Diwani wa Kata ya Igale, Michael Mwanibungu, alisema elimu iliyotolewa na maofisa wa serikali iliwahamasisha wananchi kukubali mpango huo kutokana na kuambiwa kuwa una faida kwenye matumizi yao ya ardhi.

Alisema ni vyema serikali ikapanua wigo kwa kuviingiza vijiji vingine ambavyo havijaingia kwenye mpango huo ili navyo vinufaike.

"Sisi wana Igale tumepokea mpango huu kwa mikono miwili na tunaiomba serikali iendelee kutekeleza na sisi tutatoa ushirikiano, lakini tunaomba hata vijiji vingine ambavyo havipo kwenye mpango viingizwe," alisema Mwanibungu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Horongo, Mashaka Mayasu, alisema mpango huo utawasaidia wananchi wa maeneo hayo kumiliki ardhi bila matatizo yoyote na kwamba migogoro iliyopo itamalizika.

Alisema kwa mujibu wa maelezo waliyopewa, wananchi watalipa gharama kidogo kwenye umilikaji wa ardhi na kwenye upimaji zoezi hilo linafanywa bila gharama.



# Mke wa Rais awapa somo wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, amewata wajasiriamali kuitumia vizuri elimu waliyopata ya masuala ya fedha na mikopo kwa sababu elimu hiyo ni muhimu katika kuleta mabadiliko chanya katika kupata maendeleo.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya wajasiriamali wa mkoa wa Kusini Unguja yaliyoandaliwa na Benki ya CRDB ikiwa ni ufunguzi wa tamasha la Kizimkazi, kijiji ambacho anatokea Rais Samia Suluhu Hassan.

Mama Mwinyi alisema tamasha hilo ni fursa za maendeleo kwa makundi mbalimbali hivyo mafunzo hayo ni nafasi adhimu kwao kuwajengea uwezo ili kufanya shughuli kwa ufanisi na kuwaletea tija.

Alisema Serikali ya Zanzibar iko katika hatua ya kuiunganisha pamoja mifuko ya uwezeshaji na kufanya kazi kwa ufanisi katika kuwasaidia wajasiriamali.

Kiongozi huyo aliipongeza Benki ya CRDB kwa kudhamini tamasha la Kizimkazi na kuwapongeza wananchi wa kjiji hicho kwa ubunifu wa kulianzisha.

"Tamasha hili ni ishara ya umoja na upendo na mshikamano wenu wana Kizimkazi," alisema.

Pia aliitaka Benki ya CRDB kuisaidia sekta ya elimu kwa Mkoa wa Kusini Unguja na kuzipatia vifaa shule za mkoa hizo ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi na kuchochea mabadiliko.

Aliwataka wazazi na walezi wa watoto wa mkoa huo kuwalea watoto wao katika malezi mazuri na kusoma kwa bidii ili kuwa na maendeleo mazuri.

Naye Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa, alisema Benki ya CRDB imedhamiria kubadilisha maisha ya wana Kizimkazi kupitia sera yake ya kurudisha kwenye jamii. Alisema kila mwaka benki hutenga asilimia moja ya faida yake kuwekeza katika jamii.

Sambamba na ufadhili wa tamasha la Kizimkazi, Benki ya CRDB imekamilisha ujenzi wa miradi miwili ya maendeleo ambayo itakabidhiwa kwa mgeni rasmi wa Tamasha la Kizimkazi, Rais Samia siku ya kilele cha tamasha Agosti 28, mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema tamasha la mwaka huu litakuwa la kihistoria kutokana na kupewa nguvu kubwa na Benki ya CRDB ambayo imekuwa mdau mkubwa wa Kizimkazi tangu tamasha hilo lilipoanza kama 'Samia Day' mwaka 2016.

Pamoja na shughuli hizo za kimaendeleo, utamaduni, sanaa na michezo, wananchi ambao watahudhuria tamasha la Kizimkazi watapata fursa ya chanjo ya UVIKO-19 itakayotolewa katika viwanja vya Kizimkazi Dimbani, Mji Mpya likiongozwa na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui.

# Vikao masuala Muungano vyaanza rasmi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya pamoja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoshughulikia masuala ya Muungano, inaendelea na vikao vyake Mjini Zanzibar kujadili masuala mbalimbali ya Muungano.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Selemani Jafo, Vuga mjini Unguja, alisema mawaziri na makatibu wakuu wa pande zote mbili wapo hapa kwa ajili ya kikao hicho.

Alisema baada ya kikao hicho cha mawaziri wa SMT na SMZ, wajumbe watapata fursa ya kutembelea miradi ya kimkakati ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III), na kiwanda cha maziwa cha Bakhresa huko Fumba. Alisema miradi hiyo ni miongoni mwa hoja za Muungano ambazo zimekuwa zikitafutiwa ufumbuzi na kamati ya pamoja.

Waziri Jafo alisema mwenyekiti wa kikao hicho ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango na wajumbe wengine ni pamoja na Waziri Mkuu wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

"Ni matumaini yetu kuwa kupitia vikao hivi tutapata ufumbuzi wa hoja mbalimbali zinazotukabili katika utekelezaji wa masuala ya muungano," alisema.

Jafo alisema baada ya kikao hicho kutakuwa na utiaji saini wa hati za makubaliano ya hoja zilizopatiwa ufumbuzi katika ukumbi wa Chuo cha Utalii Maruhubi.

Alisema tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa kushughulikia hoja za Muungano kupitia vikao vya kamati ya pamoja mwaka 2006, hoja 25 zimejadiliwa na mpaka sasa hoja saba tayari zimepatiwa ufumbuzi na 18 zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

Hoja mbili zilizopatiwa ufumbuzi, kwa mujibu wa Jafo, zilitiwa saini hati za makubaliano katika kikao cha mwaka 2010 na kuondolewa katika orodha ya hoja za Muungano.

Akizitaja hoja hizo kuwa ni utekelezaji wa sheria za haki za binaadamu Zanzibar na utekelezaji wa sheria ya 'mechant shipping' katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia alisema katika kikao kilichofanyika Oktoba, mwaka jana, hoja tano zilizopatiwa ufumbuzi zilitiwa saini hati za makubaliano na kuondolewa katika orodha ya hoja za Muungano.

Alizitaja hoja hizo kuwa ni ushirikishwaji wa serikali ya Zanzibar kwenye masuala ya kimataifa na kikanda, ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, gharama za kushusha mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwa mizigo inayotoka Zanzibar, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, na uratibu wa vikao vya kamati ya pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano.

Waziri Jafo alisema lengo la kuweka utaratibu huo ni kuimarisha Muungano kwa kuhakikisha kuwa changamoto zote zinapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salim, alisema majadiliano ya hoja mbalimbali yatafanyika katika vikao hivyo ili kupata ufumbuzi wa mambo mbalimbali katika Muungano.

Alisema ufumbuzi utakaopatikana utasaidia katika kuimarisha nyanja mbalimbali kwa maendeleo ya taifa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, akizungumza na waandishi wa habari, Vuga Mjini Zanzibar jana, kuhusu kikao cha kamati ya pamoja kinachoshughulikia masuala ya Muungano kinachoendelea kisiwani humo. Kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk. Sada Mkuya. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ukatili, udhalilishaji kijinsia washika kasi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VITENDO vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto vimeongezeka kwa mwezi wa Julai hali ambayo inasababisha kuharibu mustakbali mzima wa maisha ya watoto.

Akiwasilisha takwimu za ukatili za udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto Zanzibar, Ramla Hassan Pandu, kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, alisema matukio 108 yameripotiwa Julai, mwaka huu, hali ambayo imeonekana kuongezeka ikilinganishwa na Mei ambapo yaliripotiwa 97.

Alisema, Wilaya ya Magharibi 'A' inaongoza kwa kuripotiwa matukio 29 ikifuatiwa na Wilaya ya Magharibi 'B' kwa matukio 23.

Naye Mkurugenzi wa Jinsia na Watoto kutoka Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nasma Haji Chumu, alisema bado hali ya vitendo hivyo hairidhishi katika jamii na kwa sasa kumezuka wimbi kubwa la utoroshaji wa watoto wa kike kuanzia miaka 14 hadi 17.

Kutokana na hali hiyo, alisema ni vyema wazazi kuhakikisha wanawasimamia ipasavyo kwa kuhakikisha wanatambua nyendo za watoto wao kuanza shule hadi katika mitaa wanayoishi.

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Khamis Othman, alisema kwa sasa hali bado ni mbaya na kwamba kumekuwapo vitendo vingi vinavyoripotiwa katika mahakama licha ya serikali kuwa na msukumo wa kumaliza vitendo hivyo. Pia alisema vitendo vingi vinavyoripotiwa ni pamoja na kushabihiyana na utumiji wa dawa za kulevya kwa vijana ambapo kwa kiasi kikubwa vinachangia kufanya vitendo vya udhalilishaji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**A SALES PERSON IS REQUIRED**

A SALES PERSON IS REQUIRED FOR AN ESTABLISHED PHARMACEUTICAL COMPANY BASED IN DAR ES SALAAM

**CONTACT: 0713 786 300**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**KITULA NICHOLAUS MASAU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0989/0054** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule yan secondary **KIBARA HIGH** mwaka **2016,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Poliosi taarifa **BND /RB/505/2019**

116419202

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALEX DAUD** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0765-0017** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **NGANA** mwaka **2006,**yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **KAT/MPA/RB/401717/2021**

116419102

## KUPOTEA KWA CERTIFICATE

**INDEPENDENCE POWER TANZANIA LTD (IPTL)** wanatangaza kupotelewa na certificate of approval iliyotolewa nan a **TANZANIA INVESTMENT (TIC)** mwaka 20th February 1997 chenye namba 121713,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/396547/2021**

116419302

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa mirathi 82 /2021**

**Ombi la BARAKA TEOPHIL MASAMBA kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu MARIA CHACHA MRIMI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 6/09/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 20/08/2021

Tarehe 20/8/2021

Sahihi ya Hakimu

116419502

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.72 OF 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ELIZABETH ISACK KINGAMKONO**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ISACK KINGAMKONO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 13 Day of 09 2021.

**Dated at Dodoma this 4TH day of August 2021**

MAGISTRATE

116419802

**IN THE UNITED REPUPLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT COURT OF MVOMERO**
**AT MVOMERO**

**CIVIL NO.01/2021**

**THOMAS MWENYEHERI.........................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**MWINCHANDE HAJI MDIMA.........................1.DEFENDANT**
**MARIAM ALLY ABDALLAH............................2.DEFENDANT**

**(BY WAY OF COUNTERCLAIM)**

**MWINCHANDE HAJI MDIMA.........................1.PLAINTIFF**
**MARIAM ALLY ABDALLAH..............................2.PLAINTIFF**

**VERSUS**

**THOMAS MWENYEHERI..................................1.DEFENDANT**
**FRED FANUEL ELISHAWARI...........................2.DEFENDANT**

FRED FANUEL ELISHAWARI, You are ordered to appear before this court in person or represented by your advocate on 31/08/2021 in civil case NO. 1/2021 for hearing.

**Given under my seal on 19...... day 08........ 2021**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT OF MVOMERO.

116419902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMCAT T LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA **TIPPER** YENYE NAMBA USAJILI **T.144 BES.** CHASSIS NAMBA **90891** ENGINE NAMBA **M11380E34928205.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/412361/2021**

116420402

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Chakwera kupunguza bei ya mbolea Malawi

**Lilongwe,** MALAWI

RAIS wa Malawi Lazarus Chakwera amesema kwamba, atachukua hatua kudhibiti ongezeko kubwa la bei ya mbolea ambalo lilikithiri mwaka mmoja uliopita.

Kiongozi huyo amesema kuwa takriban asilimia 80 ya wakulima wa Malawi, hawawezi tena kumudu bei ya mbolea.

Wakulima wa Malawi walisema ongezeko kubwa la bei za mbolea huwenda likaathiri uzalishaji chakula, kwenye taifa hilo la kusini mwa Afrika ambalo hutegemea kilimo.

Bei za mbolea zimepanda maradufu, mfuko wa kilo 50 unauzwa kati ya dola 40 hadi 50 za kimarekani. Bei hizo ni karibu mara mbili zikilinganishwa na mwaka mmoja uliopita.

Wataalamu wa kilimo wanasema kwa hali hiyo, huwenda ikasababisha kuongezeka kwa bei za mbolea, inayotolewa kwa wakulima kupitia programu maalum ya ruzuku ya serikali kwa wakulima maskini na hulipia dola sita pekee kwa mfuko wa kilo 50.

Chakwera, mwishoni mwa wiki, kupitia televisheni ya kitaifa aliapa kuhakikisha kuwa bei za mbolea zinashuka.

Kiongozi huyo alisema kuwa ongezeko la bei ya mbolea limesababishwa na kundi la watu ambao hakuwataja majina, akisema kuwa nia yao ni kuhujumu programu ya serikali ya utoaji mbolea kwa wakulima maskini.

Chakwera alisema huwenda bei za mbolea zitapanda kidogo, ikilinganishwa na mwaka jana, kama zilivyo kwa sasa. **VOA**

# Uganda yaamuru walimu wote kuchomwa chanjo ya corona



**Kampala,** UGANDA

WAZIRI wa Elimu wa Uganda, Janet Museveni, ameamuru walimu nchini kote, kupata chanjo ya Covid-19 vinginevyo wazuiwe kuingia madarasani shule zitakapofunguliwa.

Waziri huyo ambaye ni mke wa Rais Museveni (pichani), ameonya kuwa mwalimu yeyote atakayekwenda kazini akiwa na cheti cha kughushi, kuthibitisha kuwa amechanjwa, atakuwa hatarini kupoteza kazi yake.

**Waziri huyo ambaye ni mke wa Museveni, ameonya kuwa mwalimu yeyote atakayeghushi, atakuwa hatarini kupoteza kazi yake.**

Alisema kuchanjwa kwa walimu kutasaidia kuwalinda wanafunzi, dhidi ya virusi na kuongeza kuwa vituo vya chanjo vitawekwa kwenye shule na vyuo vikuu vitakapofunguliwa.

Waziri Museveni alisema wiki za hivi karibuni kutafunguliwa tena shule, ambazo zilifungwa tarehe Juni 6, mwaka huu, ili kudhibiti maambukizi ya wimbi la pili la maambukizi ya virusi vya corona. **BBC**



Waafghanistan wakiingia kwenye ndege ya jeshi ya Marekani, wakati wakiondolewa nchini humo katika Uwanja wa Kabul. **PICHA: REUTERS**



Mwanajeshi wa Marekani akiwa na mtoto mchanga wakimsubiri mama wa mtoto huyo baada ya kuokolewa, kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Hamid Karzai nchini Afghanistan. **PICHA: REUTERS**

# Taliban yasisitiza kutoongezea muda vikosi kusalia Afghanistan

**Kabul,** AFGHANISTAN

KUNDI la Taliban limesema muda wa mwisho ni Agosti 31 wa kuondoka kwa majeshi ya nchi za Magharibi na muda hautoongezwa.

Hayo yanajiri wakati Uingereza ikitoa wito kwa Marekani, kuongeza muda wake wa kuwaondoa watu nchini humo.

Msemaji wa Taliban ametoa kauli hiyo ya kutokubali kuongeza muda huo, ingawa duru zinaarifu hakuna ofisa yeyote wa serikali za Magharibi, aliyezungumza na wanamgambo hao kuhusiana na muda huo kuongezwa.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, anapanga kumshinikiza Rais wa Marekani Joe Biden, kuhusiana na suala hilo, katika mkutano wa dharura wa nchi saba zilizostawi kiviwanda G7, leo, ambao Uingereza ndiyo iliouitisha.

Uingereza inasema bila Marekani, nchi zingine hazina budi kuondoka, ili kusitisha juhudi zake za kuwaokoa watu kutoka Afghanistan, ambayo utawala wake umechukuliwa na kundi la Taliban.

Biden hajaondoa uwezekano wa kuongeza muda huo, ingawa alisema huwenda ikawa hakutokuwa na haja ya kufanya hivyo.

"Tazama, tunashirikiana kwa karibu sana na G7. Nimezungumza na viongozi wengi wa G7. Nitafanya mkutano nao nafikiri Jumanne (leo) na tutalizungumzia suala hilo," alisema Biden.

Rais Biden pia ameelezea wasiwasi wake kuhusiana na kitisho kinachoweza kutokana na kundi la Dola la Kiislamu, wakati Jeshi la Marekani linapania kuwaondoa raia wa nchi hiyo na marafiki zake.

Biden anadai kundi hilo ni hasimu wa Taliban na kadri wanajeshi wa Marekani wanavyozidi kusalia nchini humo, ndivyo uwezekano wa Dola la Kiislamu kuwashambulia wanajeshi wa Marekani na raia wasio na hatia katika Uwanja wa Ndege wa Hamid Karzai unavyozidi kuongezeka.

Mkuu wa Sera za Kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrell, alisema karibu raia 400 wa Afghanistan waliokuwa wanafanya kazi na umoja huo, watapewa hifadhi Ulaya.

Borrell alisema kwa sasa wanapelekwa Uhispania kufanyiwa vipimo na kisha kupelekwa katika nchi tofauti za Ulaya, zilizo tayari kuwapa vibali vya kuishi nchini mwao. **DW**

HABARI MICHEZO

MECHI KALI
HOME
BARROW
6.50 | 4.73 | 1.41
ASTON VILLA
AWAY

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
halopesa
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# PIQUE AIPA PIGO BARCA



**BARCELONA,** Hispania

NAHODHA na beki wa Barcelona, Gerard Pique, alitolewa nje baada ya kupata majeraha katika kipindi cha kwanza kwenye mechi ya La-Liga dhidi ya Athletic Bilbao.

Pique alitua chini vibaya baada ya kuruka hewani kuwania mpira dhidi ya Alex Berenguer na kumsababishia kupata maumivu katika nyama za paja na nafasi yake kuchukuliwa na Ronald.

Kocha wa Barcelona, Ronald Koeman alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari kabla ya mechi, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alikuwa akisumbuliwa na maumivu kiasi, lakini alifanya mazoezi kama kawaida wiki hii.

Hii ni mara ya sita kwa Pique kutolewa katika mechi 13 za mwisho za LaLiga, ambayo ni idadi sawa ya nyakati ambazo alibadilishwa katika mechi zake 111.

Baada ya mchezo huo, Barcelona ilithibitisha kwamba Pique alikuwa na shida ya nyama za paja na atapimwa ili kujua ukubwa wa jeraha hilo.

Kuna uwezekano mkubwa wa Pique kuwa nje ya dimba kwa angalau wiki mbili au tatu.



# *Mourinho amjaza sifa Abraham*

**ROME,** Italia

JOSE Mourinho amemsifia Tammy Abraham kama "mchezaji muhimu" baada ya mshambuliaji huyo kutoa pasi za mwisho mbili wakati AS Roma ikishinda mabao 3-1 dhidi ya Fiorentina, juzi Jumapili.

Bao la ufunguzi la Henrik Mkhitarayan lilisawazishwa na Nikola Milenkovic, lakini Jordan Veretout akafunga mara mbili kuiwezesha Roma kuibuka na ushindi huo.

Abraham alitoa pasi mbili za mwisho kwa Mkhitaryan na Veretout kwenye mchezo wake huo wa kwanza kuichezea klabu hiyo.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Chelsea, alitoa pasi moja ya mwisho tu katika mechi zake 42 za Ligi Kuu akiwa na Chelsea msimu uliopita.

"Kwa uhakika Tammy (Abraham) alionyesha kiwango cha kuvutia," alisema Mourinho akiiambia DAZN baada ya mchezo huo.

"Kwa wakati huu, anaonekana atakuwa msaada na mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi chetu, nina uhakika kwa hilo.

LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA

PAKUA SASA



# ARTETA: ARSENAL INA HALI MBAYA

**LONDON,** England

ARSENAL ipo kwenye "hali ngumu na isiyokubalika" baada ya rekodi yao ya kuanza vibaya msimu, kwa mujibu wa Mikel Arteta.

Baada ya kufungwa mabao 2-0 na Brentford na kisha Chelsea juzi, Arsenal imepoteza mechi zake mbili za ufunguzi za Ligi Kuu bila kufunga bao kwa mara ya kwanza katika historia yao.

"Sidhani kama klabu hii katika historia yake imewahi kukumbana na jambo hili," alisema Arteta akiiambia BBC Sport.

"Tunatakiwa kukabiliana na changamoto. Ligi na msimamo huwa hauamuliwa Agosti. Kitu kibaya unachoweza kufanya ni kurusha taulo. Hatuwezi kufanya hivyo."

Romelu Lukaku katika mchezo wake wa kwanza tangu ajiunge na Chelsea kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 97.5 na Reece James walifunga mabao hayo.

Arsenal sasa ipo kwenye mstari wa kushuka daraja ikiwa ni kwa mara ya kwanza kuwa katika hali hiyo kwenye mechi za ufunguzi wa Ligi Kuu tangu Agosti 1992.

Arteta aliongeza: "Unatakiwa kuelewa hali jinsi ilivyo. Tunawakosa wachezaji tisa na ni ngumu. Si tu wachezaji tisa kuna baadhi ya wachezaji wakubwa."

Walikuwa bila nyota wao, Pierre-Emerick Aubameyang na Alexandre Lacazette - pamoja na Willian na magolikipa, Alex Runarsson kwa sababu ya maambukizi ya virusi vya corona kwenye mchezo dhidi ya Brentford.



# Ancelotti akasirishwa na sare Real Madrid

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti alionekana kukasirishwa baada ya timu yake kulazimishwa sare ya mabao 3-3 na Lavante kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, juzi.

Madrid walionekana kutawala mchezo wakati walipokuwa wanaongoza kwa 1-0 baada ya Gareth Bale kufunga bao lake la kwanza la LaLiga tangu mwaka 2019, lakini wakaruhusu mabao mawili ndani ya dakika 12 na kujikuta wakiwa nyuma kwa mabao 2-1.

Vinicius Junior alisawazisha dakika ya 73 kabla ya Rober kuwaweka tena Levante mbele na Mbrazil huyo akawarudisha tena Madrid mchezoni dakika tano baadaye.

"Ulikuwa ni ujinga, baada ya kutawala mchezo kipindi cha kwanza," alisema Ancelotti akiliambia gazeti la Marca.

"Tumeachia pointi tatu ugenini baada ya kuwa na kiwango bora katika kipindi cha kwanza.

"Ni ngumu kuelezea, tunatakiwa kubadilika na kuwa makini. Tumeondoka tukiwa hatuna kiwango bora na matokeo mazuri."

'Los Blancos' hao walianza LaLiga kwa ushindi mtamu wa mabao 4-1 ugenini dhidi ya Alaves, lakini juzi wakajikuta wakikamtwa na Levante.

"Kipindi cha kwanza kilikuwa kizuri sana," aliongeza kusema Ancelotti raia huyo wa Italia.


# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 24 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3443 | Gwangju vs Seongnam Ilhwa | 2.62 | 2.91 | 2.71 |
| 15:00 | 1807 | Ararat Yerevan vs FC Noravank | 1.23 | 6.20 | 11.00 |
| 15:00 | 5352 | Coventry U23 vs Colchester U23 | 1.43 | 4.45 | 5.81 |
| 15:30 | 2991 | Barnsley U23 vs Charlton U23 | 1.77 | 3.85 | 4.30 |
| 18:00 | 1571 | Pyunik Yerevan vs Van Yerevan | 2.04 | 3.30 | 3.70 |
| 18:00 | 1642 | Tshakhuma vs Orlando Pirates | 5.11 | 2.95 | 1.84 |
| 18:00 | 5855 | Chippa Utd vs Mamelodi Sundowns | 6.30 | 3.64 | 1.55 |
| 18:30 | 3822 | Wadi Degla vs Ceramica Cleopatra | 2.42 | 2.90 | 3.15 |
| 20:00 | 1154 | Verl vs Eintracht Braunschweig | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 20:00 | 1187 | Waldhof Mannheim vs Meppen | 1.89 | 3.84 | 3.44 |
| 20:00 | 3842 | Gais vs Jonkopings Sodra | 2.80 | 3.30 | 2.50 |
| 20:00 | 5130 | Hallescher vs Kaiserslautern | 2.85 | 2.90 | 2.60 |
| 20:00 | 5392 | Zwickau vs Viktoria Berlin | 2.31 | 3.30 | 2.90 |
| 20:00 | 5394 | 1860 Munich vs Viktoria Koln | 1.73 | 3.69 | 4.33 |
| 21:00 | 1192 | Kordrengir vs Thor Akureyri | 1.76 | 3.98 | 3.64 |
| 21:00 | 1287 | UMF Selfoss vs Afturelding | 2.10 | 3.89 | 2.77 |
| 21:00 | 1920 | Scunthorpe vs Manchester City U21 | 2.85 | 3.60 | 2.30 |
| 21:00 | 3065 | Sheffield United U23 vs Swansea U23 | 1.45 | 4.56 | 5.43 |
| 21:00 | 3363 | Swansea vs Plymouth | 1.66 | 3.74 | 4.83 |
| 21:00 | 3790 | Norwich City vs Bournemouth | 1.97 | 3.50 | 3.55 |
| 21:00 | 4117 | IF Vestri vs Vikingur Olafsvik | 1.33 | 5.42 | 6.39 |
| 21:00 | 5172 | Oldham vs Accrington | 3.00 | 3.74 | 2.11 |
| 21:00 | 5865 | Exeter vs Chelsea U21 | 2.30 | 3.43 | 2.71 |
| 21:45 | 1171 | Millwall vs Cambridge Utd | 1.39 | 4.64 | 7.11 |
| 21:45 | 1368 | Huddersfield vs Everton | 5.34 | 3.91 | 1.58 |
| 21:45 | 1426 | Blackpool vs Sunderland | 2.23 | 3.46 | 2.96 |
| 21:45 | 1597 | Cardiff vs Brighton | 3.21 | 3.36 | 2.14 |
| 21:45 | 2162 | Gillingham vs Cheltenham | 2.41 | 3.44 | 2.71 |
| 21:45 | 2173 | QPR vs Oxford Utd | 1.82 | 3.85 | 3.75 |
| 21:45 | 2487 | Brentford vs Forest Green | 1.42 | 4.65 | 6.33 |
| 21:45 | 2545 | Birmingham vs Fulham | 3.31 | 3.36 | 2.10 |
| 21:45 | 2752 | Wigan vs Bolton | 2.14 | 3.36 | 3.21 |
| 21:45 | 2778 | Shrewsbury vs Rochdale | 1.91 | 3.61 | 3.66 |
| 21:45 | 3062 | Lancaster City vs Stalybridge | 2.02 | 3.48 | 3.19 |
| 21:45 | 3166 | Leeds vs Crewe | 1.37 | 4.92 | 7.09 |
| 21:45 | 3339 | Barrow vs Aston Villa | 6.50 | 4.73 | 1.41 |
| 21:45 | 3523 | Buxton FC vs Mickleover Sports | 1.91 | 3.53 | 3.48 |
| 21:45 | 3982 | Morecambe vs Preston | 3.55 | 3.30 | 2.04 |
| 21:45 | 4718 | Leyton Orient vs Harrogate | 2.10 | 3.34 | 3.29 |
| 21:45 | 4752 | Sheffield Utd vs Derby | 1.68 | 3.80 | 4.64 |
| 21:45 | 5333 | Stoke City vs Doncaster | 1.56 | 4.04 | 5.31 |
| 21:45 | 5488 | Ashton Utd vs Whitby Town | 2.50 | 3.47 | 2.46 |
| 21:45 | 5837 | Watford vs Crystal Palace | 2.48 | 3.27 | 2.73 |
| 21:45 | 5919 | Stevenage vs Wycombe | 3.29 | 3.19 | 2.18 |
| 21:45 | 5967 | Northampton vs AFC Wimbledon | 2.75 | 3.14 | 2.55 |
| 21:45 | 5994 | Gainsborough vs Scarborough Athletic | 2.57 | 3.48 | 2.39 |
| 22:00 | 2790 | Nottingham vs Wolverhampton | 3.95 | 3.16 | 1.98 |
| 22:00 | 3278 | Ferencvaros TC vs BSC Young Boys | 3.20 | 3.90 | 2.04 |
| 22:00 | 3561 | Ludogorets Razgrad vs Malmo | 2.50 | 3.36 | 2.76 |
| 22:00 | 4923 | PSV Eindhoven vs Benfica | 1.97 | 3.65 | 3.60 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AONDOA HOFU POGBA KUONDOKA UNITED

●●● Sina wasiwasi wowote, ninatarajia atakuwa hapa wakati Septemba itakapoanza...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesisitiza kiungo wa klabu hiyo, Paul Pogba hataondoka Old Trafford kwenye dirisha la uhamisho la majira haya ya joto.

**Pogba anaendelea kuhusishwa na kuondoka Old Trafford wakati Paris Saint-Germain ikiripotiwa kumtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.**

Mchezaji huyo yupo mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake na United, na Solskjaer alisema Julai kuwa klabu hiyo ilikuwa katika mazungumzo ya kumpa mkataba mpya wa muda mrefu.

"Ndio, ninatarajia Paul atakuwa hapa wakati Septemba itakapoanza," alisema Solskjaer aliwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo wake wa sare ya bao 1-1 na Southampton kwenye mechi ya Ligi Kuu ya England juzi.

"Ikiwa una mkataba wa miaka mitano au wa mwaka mmoja, wakati unatia saini Manchester United lazima upate changamoto ya kufanya kwa kiwango sawa."

"Sina wasiwasi wowote kwamba urefu wa mkataba wa mchezaji yeyote unabadilisha kiwango cha motisha na kiwango chake."

"Unatakiwa kucheza vizuri kwa timu yako, wachezaji wenzio, wewe mwenyewe, na familia yako, kila wakati unapocheza." "Ninatarajia kwamba, mtazamo wa kila mchezo ndio sahihi. Kwamba tunazingatia mwelekeo sahihi, taaluma sahihi, pamoja na hayo, sina wasiwasi wowote juu ya Paul."

## ZISIKUPITE

### HATIMA YA KANE WIKI HII

MANCHESTER City wanatarajia kupeleka ofa ya mwisho kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane wiki hii. Hatma ya nahodha huyo wa England, ambaye aliingia akitokea benchi kwenye mechi dhidi ya Wolves, haieleweki huku Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy, akitaka kumbakiza Muingereza huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Telegraph)***

### SPURS WAMTAKA TRAORE

KLABU ya Tottenham Hotspur wanaangalia uwezekano wa kupeleka ofa ya pauni milioni 40 kwa ajili ya winga wa Wolves, Adam Traore wakati huu ambapo kocha wa Spurs, Nuno Espirito Santo, akitaka kuungana na nyota huyo wa kimataifa wa Hispania, ambaye alimnoa kule Molineux kwa miaka mitatu. ***(Telegraph)***

### HAALAND NA MAN UNITED

MANCHESTER United imepata nguvu zaidi katika mbio zao za kumuwania mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, ambaye kipengele cha mkataba wake kinachotaka dau la pauni milioni 64, ili kumuuza kitaanza kufanya kazi Januari. ***(Marca)***

### SPURS WAMTAKA AOUAR

KLABU ya Tottenham Hotspur bado inamtaka kiungo wa Lyon na Ufaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 23, ambaye anatakiwa pia na Juventus. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL ILIVYOMKOSA MANUEL

ARSENAL ilishindwa kumsajili Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 23, kabla ya kiungo huyo wa Italia kujiunga na Juventus kwa mkataba wa mkopo wa miaka miwili, licha ya kutoa ofa kubwa ya fedha kwa Sassuolo kuliko magwiji hao wa Serie A, hiyo ni kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Giovanni Carnevali. ***(Gazzetta di Modena)***

### MADUEKE KUCHOMOLEWA PSV

KLABU ya Tottenham Hotspur inamuwania kiungo mshambuliaji wa timu ya Taifa chini ya miaka 21 ya England, Noni Madueke, lakini PSV Eindhoven imewaambia wakali hao wa London, kwamba itawagharimu dau la pauni milioni 40, ili kumsajili kinda huyo, ambaye aliondoka Spurs na kujiunga na klabu hiyo ya ligi ya Uholanzi ya Eredivisie mwaka 2018. ***(Mirror)***

### SARR KUTUA TOTTENHAM

TOTTENHAM Hotspur pia inataka kumsajili kiungo wa Senegal, Pape Matar Sarr mwenye umri wa miaka 18 kutoka Metz, huku Rais wa klabu hiyo ya Ufaransa, Bernard Serin, akithibitisha kwamba wako kwenye mazungumzo ya mwisho na klabu hiyo ya Ligi Kuu England kuhusu uhamisho huo, utakaogharimu zaidi ya pauni milioni 11. ***(Le Republicain Lorrain)***

### XHAKA YUPO SANA ARSENAL

MMILIKI wa Arsenal, Stan Kroenke, amethibitisha kwamba Granit Xhaka ametia saini mkataba mpya wa kuendelea kuitumia klabu hiyo. Kiungo huyo wa Uswisi aliyekuwa akihusishwa na mipango ya kuhamia AS Roma, ametia saini mkataba wa muda mrefu, kwa mujibu wa Kroenke. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# SERIKALI YAWEKA KIPORO USAJILI 'MAPRO' 12 LIGI KUU

**Na Saada Akida**

LICHA ya klabu kubwa nchini Simba, Yanga na Azam FC kupokea kwa mikono miwili ruksa ya kusajili wachezaji 12 wa kigeni kuanzia msimu huu, serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT), imesema bado haijatoa tamko lolote kuhusu ongezeko hilo.

Kwa mujibu wa kanuni za msimu uliopita, kila klabu ya Ligi Kuu iliruhusiwa kusajili wachezaji 10 wakigeni huku ikiruhusiwa kuwachezesha wote katika mchezo mmoja, lakini msimu huu Shirikisho la Soka nchini (TFF) kupitia Bodi yake ya Ligi (TPLB), imefanyia marekebisho kanuni zake ambapo sasa kila klabu inaweza kusajili 'mapro' 10 wakigeni lakini ikiruhusiwa kuwachezesha nane tu katika mchezo mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Uhusiano wa BMT, Najaha Bakari, alisema walipokea barua ya maombi ya ongezeko hilo kutoka TFF, lakini bado serikali haijatoa majibu yoyote kukubali au kukataa.

**Alisema awali walipokea maombi kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu kuongezeka kwa idadi ya wachezaji wakigeni na wakiwa kwenye mchakato huo wa kufanyia kazi mapendekezo hayo, walishangazwa kuona TFF tayari imeshatoa maamuzi kabla ya majibu kutoka.**

"Ni kweli TFF walileta barua ya maombi kwetu juu ya kuhitaji kuongeza idadi ya wachezaji wa kigeni kuwa 12, lakini kabla ya serikali kutoa tamko kuhusu hilo, wameanza mchakato huo na timu tayari zimesajili nyota hao ambao nane wataruhusiwa kucheza katika mechi mmoja wa ligi," alisema Najaha.

Alisema serikali itatoa tamko rasmi kuhusu idadi hiyo ya wachezaji 12 baada ya kumalizika kwa mchakato ambao walifanya kupitia wadau mbalimbali kupata maoni yao kuhusu usajili wa idadi ya nyota hao kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati huo huo, BMT imeweka wazi kuwa Oktoba 16, mwaka huu, ndiyo siku Chama cha Mpira wa Netiboli Tanzania (CHANETA) kinatarajia kufanya uchaguzi wa viongozi wao, ambao utafanyika, Makao Mkuu ya nchi, jijini Dodoma.

Bakari alisema fomu zimeanza kutolewa jana na mchakato huo utaendelea hadi Oktoba 12, katika Ofisi za BMT zilizopo Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam huku usaili ukitarajiwa kufanyika Oktoba 15, mwaka huu.

WIKI YETU...




Kikundi cha Yanga cha Ushangiliaji Makao Makuu Iringa Miyomboni, kikisherehekea kwa vifijo na furaha tele baada ya kuzinduliwa rasmi kwa Wiki ya Mwananchi juzi, itakayofikia kilele Agosti 29, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## *Biashara kutafutia pumzi ya CAF Mwanza*

**Na Saada Akida**

WAKATI wawakilishi wengine watatu wa nchi kwenye michuano ya kimataifa wakiweka kambi nje ya nchi kujiwinda na msimu mpya, uongozi wa Biashara United, umesema kutokana na changamoto ya muda wa maandalizi wa timu hiyo kuwa mfupi, wataendelea kujichimbia jijini Mwanza.

Simba na Yanga zinazoiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, zimeweka kambi nchini Morocco wakati Azam FC itakayoipeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika pamoja na Biashara United, yenyewe juzi usiku ikikwea pipa kuelekea Zambia kwa maandalizi.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, alisema mipango yao ya awali ilikuwa ni kuipeleka timu hiyo nchini Kenya kuweka kambi, lakini kwa sababu ya muda mfupi wa kujiandaa na mechi yao dhidi ya FC Dikhil ya Djibouti, hawataweza kufanya hivyo tena.

Alisema wakiwa Mwanza watahakikisha wanapata timu kutoka hapa nchini ambazo watacheza mechi za kirafiki zenye ushindani kujiweka imara kwa ajili mchezo huo lengo lao likuwa ni kuvuka katika hatua ya awali kwenye michuano hiyo ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

"Tumeingia kambini hapa Mwanza na tunaendelea kutafuta timu za hapahapa nchini, kucheza nazo mechi za kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mechi yetu dhidi ya FC Dikhil, muhimu sana kwetu kutafuta matokeo mazuri ugenini," alisema Mataso.

Alisema wanatambua mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu watakuwa ugenini, lakini watatumia mechi hizo za kirafiki kujiandaa vizuri kwenda kupata matokeo chanya. Biashara United imepangwa kuanzia ugenini na FC Dikhil ya Djibout kati ya Septemba 10 hadi 12, mwaka huu na iwapo itafanikiwa kupenya katika michezo yao miwili ya awali, inavaana na mshindi kati ya Hay Al-Wadi ya Sudan na Ahli Tripoli ya Libya.

Biashara United imepata nafasi hiyo baada ya kumaliza katika nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi Kuu Bara msimu uliopita nyuma ya mabingwa Simba, Yanga na Azam FC iliyomaliza nafasi ya tatu.

## Ndayiragije apanda, Minziro akishushwa

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

NI rasmi sasa Geita Gold FC ya mkoani Geita inayojianda kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu mpya wa 2021/22, imeingia mkataba wa mwaka mmoja na kocha Etienne Ndayiragije raia wa Burundi huku ikimshusha aliyekuwa Kocha wake Mkuu, Felix Minziro kuwa msaidizi wake.

Uamuzi huo umewekwa wazi na Mwenyekiti wa timu hiyo, George Beligenda, wakati akimtambulisha rasmi Ndayiragije juzi, ambapo alisema kuanzia sasa Minziro atakuwa kocha msaidizi.

"Tumeingia kandarasi ya mwaka mmoja na Etienne Ndayiragije kuwa kocha mkuu wa timu ya Geita Gold FC, kocha aliyekuwapo awali, Felix Minziro 'Baba Isaya' [ambaye ameipandisha Ligi Kuu], atabaki katika timu hii kama kocha msaidizi," alisema mwenyekiti huyo.

Kuhusu usajili, mwenyekiti huyo alisema mpaka sasa wamesajili wachezaji 25 wenye uwezo mkubwa kutoka klabu mbalimbali ikiwamo baadhi kutoka Klabu ya Yanga.

## Mbeya Kwanza yasajili kifaa kutoka Mamelodi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya Kwanza ambayo itacheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu, imeendelea na usajili kukiimarisha kikosi chao, baada ya kumsajili mchezaji Habib Kyombo kutoka Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Kyombo, mchezaji wa zamani wa Mbao FC na Singida United, amesajiliwa na timu hiyo kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Mtandao rasmi wa klabu hiyo, umeeleza kuwa wamemsajili mchezaji huyo aliyekuwa akichezea kwa mkopo Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, akitokea Singida United.

"Rasmi, tumemkaribisha kwenye familia yetu, mchezaji Habib Kyombo, Mtanzania aliyekuwa anachezea Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwa mkopo. Karibu nyumbani mshambuliaji Kyombo."

Mchezaji huyo alikwenda Sauzi msimu wa 2018/19, lakini hakuichezea sana klabu yake hiyo, kutokana na kukumbwa na majeraha na kwa muda mrefu aliutumia kwenye chumba cha matibabu, badala ya uwanjani.

# Michezo

Jumanne Agosti 24, 2021

Nipashe




## Solskjaer aondoa hofu Pogba kuondoka

UKURASA 22

## NGUMU KUMEZA!...



Bondia mkongwe, Mfilipino Manny Pacquiao akichapwa konde la uso na Mcuba, Yordenis Ugas katika pambano la kuwania ubingwa wa WBA uzito wa Super Welter lililofanyika T-Mobile Arena jijini Las Vegas, Marekani juzi. Ugas alishinda kwa pointi. **PICHA: MTANDAO**

## Arteta: Arsenal ina hali mbaya

**LONDON,** England

ARSENAL ipo kwenye "hali ngumu na isiyokubalika" baada ya rekodi yao ya kuanza vibaya msimu...



HABARI UK. 21

## Serikali yaweka kiporo usajili 'mapro' 12 Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

LICHA ya klabu kubwa nchini Simba, Yanga na Azam FC kupokea kwa mikono miwili ruksa ya...

HABARI UK. 23

# Corona yatajwa kambi Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Wachezaji wachache warejea, kukipiga na Zanaco kilele cha Siku ya Mwananchi...

KLABU ya Yanga imesitisha kambi yake nchini Morocco kwa sababu mbalimbali na baadhi ya wachezaji wakirejea Tanzania jana huku wengine wakilazimika kusalia nchini humo.

**Miongoni mwa sababu zilizotajwa na uongozi wa Yanga ni idadi ya wachezaji kupungua baada ya baadhi kwenda kujiunga na timu zao za taifa kwa ajili ya mechi za kuwania kufuzu Kombe la Dunia mapema mwezi ujao.**

Lakini kwa taarifa zilizolifikia gazeti hili kutoka chanzo chetu ndani ya kambi hiyo iliyopo jijini Marrakech, Morocco na vyonzo vyetu hapa nchini, zimedai kwamba kuna baadhi ya wachezaji wamekutwa na maambukizi ya virusi vya corona na hao hawatarejea kwani watalazimika kubaki karantini kwa wiki moja.

"Kuna wachezaji 14, wamepata maambukizi ya virusi vya corona na si 19 kama ambavyo baadhi ya taarifa zinadai, hivyo wametakiwa kukaa karantini kwa wiki moja," kilieleza chanzo chetu na kuomba hifadhi ya jina lake.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili, Mhandisi Hersi Said, aliyeko kambini nchini Morocco na timu hiyo, alipoulizwa sababu ya kuvunja kambi na kurejea kwa mafungu, alisema ni kutokana na ratiba ya ndege.

"Ni kweli tumelazimika kuvunja kambi na timu ilitakiwa kurudi kwa pamoja, lakini kwa sababu ya tatizo la kubadilisha tiketi kuna watakaorudi leo [jana] na wengine tarehe 27," alisema.

Wakati Hersi akiyasema hayo, taarifa iliyotolewa na klabu hiyo kwa vyombo vya habari jana ilieleza: "Uongozi wa Klabu ya Yanga unapenda kuutaarifu umma kwamba umeamua kusitisha kambi ya msimu (Pre-season) na timu itarejea leo (jana).

"Awali, timu ilipanga kuwa na kambi ya siku 10 za mazoezi, ambazo zilikuwa zikamilike Agosti 27, lakini kutokana na sababu mbalimbali na kwa maslahi mapana ya klabu, uongozi umeamua kuchukua hatua ya kusitisha kambi hiyo na maandalizi yataendelea kambini Avic Town."

Katika taarifa hiyo, pia ilieleza kuwa klabu hiyo itafanya uzinduzi wa jezi mpya za msimu ujao Jumatano wiki hii na baada ya uzinduzi huo, zitapatikana madukani kwa ajili ya wapenzi, mashabiki na wanachama kununua.

"Uongozi unawaomba, wanachama, wapenzi na mashabiki kuendelea kuhamasishana kwa ajili ya Wiki ya Mwananchi ambayo kilele chake kitakuwa Agosti 29, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa," ilieleza.

Lakini Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alimwambia mwandishi wetu: "Sisi taarifa yetu imejikita katika suala hilo na katika taarifa yetu ipo wazi, huu ugonjwa upo dunia nzima na si jambo la ajabu, sisi tunasisitiza kila mtu kujikinga kwani hata wachezaji kubwa wanaupata.

"Kama kuna kuna kitu kama hicho basi Yanga inapaswa kupongezwa kwa kuchukua hatua mapema ya kufanya maamuzi hayo, sisi tunachoweza kusema ni kila mtu kujikinga na kuchukua tahadhari na tunasisitiza mashabiki watakaokuja Siku ya Mwananchi kujikinga kwa kuvaa barakoa," alisema Bumbuli.

Aidha, Bumbuli alisema siku ya kilele cha Mwananchi timu hiyo itacheza dhidi ya Zanaco ya Zambia.

Yanga iliweka kambi nchini humo kujiandaa na msimu mpya hususan kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Rivers United itakayochezwa kati ya Septemba 10-12, mwaka huu ikiwa ni zaidi ya wiki mbili kabla ya Ligi Kuu Bara kuanza.

Ligi Kuu Bara itaanza Septemba 29 ikiwa ni siku nne baada ya Simba na Yanga kufungua pazia la ligi hiyo kwa kucheza mechi ya Ngao ya Jamii itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042